Haliuzwi

DESEMBA 15, 2025

/islamicftz

Jumada II 24 1447

IMAAN

ISSN 5618 - NO. 562

Huwatoa watu gizani kwa idhini ya Allah

Rais Mwinyi: Tuendelee kuiombea nchi amani na utulivu

Wasifu wa masheikh wa Kongamano Misk ya Roho

Uganda yazindua bima ya Takaful

Uhaba mkubwa maji wakumba mikoa sita

Wakazi wa mikoa ya Dar es Salaam, Simiyu, Pwani, Morogoro, Dodoma na Arusha wanakabiliwa na uhaba mkubwa wa maji, unaotajwa kuwa miongoni mwa mikubwa zaidi katika miaka ya karibuni

Tujifunze kutoka historia athari za vurugu za kisiasa

Serikali yaipongeza Saudi Arabia kufadhili masomo kwa Watanzania

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, akiwa na Balozi wa Saudi Arabia, Yahya Bin Ahmed Okeish, ambapo wamejadili kuimarisha ushirikiano katika sekta ya elimu pamoja na kuongeza fursa za skolashipu kwa vijana

Trump ashambuliwa kila kona kwa kuita Wasomali takataka


Kongamano La 4 La
Afrika Mashariki
Diamond Jubilee
Disemba
27
MUHAMMAD
صلى الله عليه وسلم
“MSINGI
WA AMANI”



Na Ukhti Fatima Ss

Wasifu wa masheikh wa Misk ya Roho

Zikiwa zimebaki siku kumi na ushee kabla ya kufanyika kwa Kongamano la Misk ya Roho litakalofanyika jijini Dar es Salaam, waandaaji wameweka wazi wasifu wa masheikh sita watakaowasilisha mada katika kongamano hilo.

Kongamano la mwaka huu linatajwa kuwa la kipekee, likiwa limebeba sura mpya ya ulinganiaji wa dini kwa kuwapa nafasi masheikh vijana, hatua inayolenga kuifikia kwa karibu zaidi kizazi cha sasa hususan vijana wa Gen Z.

Masheikh hao kutoka Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi watazungumzia mada mbalimbali zinazojikita katika kauli mbiu ya kongamano hilo isemayo "Mtume Muhammad (amani ya Allah imshukie), msingi wa amani", kwa matumaini kuwa ujumbe huo utakuwa mwongozo sahihi kwa wananchi wa ukanda huu na hasa vijana wanaokabiliwa na changamoto za misimamo mikali, mmomonyoko wa maadili na migawanyiko ya kijamii.

Sheikh Abdallah Abdulkadir Al-Ahdal – *Tanzania*

Sheikh Abdallah Abdulkadir Al-Ahdal ni msomi wa Kiislamu na mhubiri kijana mwenye ushawishi mkubwa katika jamii, hususan miongoni mwa vijana. Ni mhitimu wa Shahada ya Kwanza ya Sharia kutoka Chuo Kikuu cha Kiislamu cha Madina na anaendelea na masomo ya Uzamili katika Fiqh na Usul al-Fiqh, akibobea katika masuala ya mirathi ya Kiislamu (al-Mawarith). Pia anamiliki ijaza mbalimbali katika Qur'an, Hadith na Fiqh, hali inayompa uhalali wa kitaaluma katika kazi yake ya da'wah.

Kwa sasa, Sheikh Al-Ahdal anahudumu kama Makamu Mkuu wa Maahad Al-Hikma, Dar es Salaam, ambapo anasimamia masomo, walimu na malezi ya wanafunzi.

Aidha, ni mhadhiri katika Msikiti wa Nuurulhikma na mshauri wa kidini katika kituo cha televisheni cha Al-Haajar TV, nafasi inayompa fursa ya kufikia jamii pana kupitia vyombo vya habari.

Katika Kongamano la Misk ya Roho, Sheikh Al-Ahdal anatarajiwa kuweka msingi wa mjadala kwa kuzungumzia nafasi ya Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) katika kujenga amani, mada inayolenga kufungua uwanja wa tafakuri kwa masheikh wengine na kuwasaidia washiriki kuelewa mizizi ya amani katika Uislamu.

Sheikh Abdulkhaliq Issa Kassim – *Kenya*

Sheikh Abdulkhaliq Issa Kassim ni miongoni mwa masheikh vijana wanaovutia umakini kutokana na safari yake ya kipekee inayounganisha taaluma ya kisasa na ulinganiaji wa Kiislamu.

Mbali na elimu ya dini, Sheikh Abdulkhaliq amepitia masomo ya masuala ya anga (aviation) na kuidhinishwa kama rubani wa ndege, taaluma iliyomjengea nidhamu, uwajibikaji na umakini mkubwa katika maisha.

Alianza safari yake ya kielimu katika Abu Hureira Academy mjini Mombasa, ambako alihitimu elimu ya sekondari, kabla ya kujiunga na Chuo Kikuu cha Mount Kenya kusomea Shahada ya Usimamizi wa Biashara.Ingawa mazingira hayakumruhusu kukamilisha shahada hiyo, kipindi hicho kiliweka msingi muhimu wa mtazamo wake uliosawazika kati ya masuala ya kidunia na malengo ya kidini.

Safari yake ya kiroho ilimfikisha katika Mji Mtukufu wa Madina, ambako alipata fursa ya kujifunza kwa kina Qur'an, Sunna na misingi ya da'wah chini ya Wanazuoni wanaoheshimika. Uzoefu huu ulimwezesha kuunganisha elimu ya dini na uhalisia wa maisha ya kisasa, hasa changamoto zinazowakabili vijana.

Kupitia Kongamano la Misk ya Roho, Sheikh Abdulkhaliq anatarajiwa kuzungumzia namna Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) alivyokuwa mfano wa kuigwa katika kulinda amani na nidhamu, akilenga kuwahamasisha vijana kuwa raia wema, wenye mchango chanya katika jamii na wanaoishi Uislamu kwa vitendo.

Sheikh Abubakar Misigaro – Burundi

Sheikh Abubakar Misigaro ni mhubiri wa Kiislamu kutoka Burundi mwenye uzoefu mpana wa kielimu na kiutendaji katika nyanja za da'wah na elimu. Ni mhitimu wa Shahada ya Kwanza ya Sharia kutoka Chuo Kikuu cha Kiislamu cha Madina na Shahada ya Uzamili ya Fiqh kutoka Chuo Kikuu cha Kiislamu cha Minnesota.

Amehudumu kama mhubiri chini ya Wizara ya Elimu ya Saudi Arabia kwa zaidi ya muongo mmoja, sambamba na kuwa Mkuu wa Shule ya Kiislamu ya Maahad Nur, Kiyange. Pia ni mjumbe wa Baraza la Kitaifa la Masheikh nchini Burundi na Mshauri wa Masuala ya Kiislamu katika Benki ya KCB Sahal, Bujumbura.

Katika kongamano hilo, Sheikh Misigaro anatarajiwa kufafanua ujumbe wa amani uliomo ndani ya Qur'an na Sunna, akionesha namna misingi hiyo ya Kiislamu inavyoweza kuwa suluhisho la migogoro na misukosuko ya kijamii inayoshuhudiwa katika jamii za leo.

Sheikh Hassan Nsanzimana bin Abdulshakur – *Rwanda*

Sheikh Hassan Nsanzimana ni msomi wa Qur'an na Qira'at kutoka Rwanda, anayeheshimiwa miongoni mwa wanazuoni wachache waliobobea katika fani hiyo. Ni mhitimu wa Shahada ya Sharia kutoka Chuo Kikuu cha Kiislamu cha Madina, mhifadhi wa Qur'an na mwenye ijaza ya Qira'at kumi.

Amehudumu kama mwalimu wa Qur'an katika Rwanda na Kenya, mjumbe wa Baraza la Wanazuoni Rwanda, pamoja na Mwenyekiti wa Kamati ya Majaji wa Mashindano ya Kimataifa ya Qur'an ya Rwanda. Pia ameshiriki katika uongozaji na uelimishaji wa mahujaji

MUHAMMAD صلى الله عليه وسلم "MSINGI WA AMANI"

Na Ukhti Fatima Ss

Wasifu wa masheikh wa Misk ya Roho

na waumra katika mji wa Madina.

Kupitia Kongamano la Misk ya Roho, Sheikh Hassan anatarajiwa kuzungumzia uhusiano kati ya Qur'an, uchumi na amani ya Muislamu, akilenga kuonesha namna maadili ya Qur'an yanavyoweza kuleta uwiano na utulivu katika maisha ya kijamii na kiuchumi.

Sheikh Hassan Mohamed Mohamed – *Tanzania*

Sheikh Hassan Mohamed Mohamed ni msomi na mhubiri wa Kiislamu kutoka Tanzania, mzaliwa wa Mkoa wa Tanga, mwenye uzoefu mrefu katika elimu ya dini na ufundishaji. Kielimu, Sheikh Hassan ni mhitimu wa Shahada ya Uzamili ya Tafsiri na Sayansi ya Qur'an kutoka Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Afrika kilichopo Sudan, alichosoma kati ya mwaka 2015 na 2017.

Kabla ya hapo, alihitimu Shahada ya Masomo ya Kiislamu kutoka College of Islamic Studies nchini Kenya, hatua iliyomjengea msingi imara katika taaluma za dini na ulinganiaji.

Hata hivyo, safari yake ya elimu ilianza mapema katika kituo cha elimu cha Kiislamu vya Amkeni Islamic Center nchini Kenya, ambako alipata elimu ya awali, elimu ya sekondari na ya sekondari ya juu ya dini, sambamba na kuhifadhi Qur'an Tukufu. Aidha, amepitia mafunzo ya ziada ikiwemo kozi ya lugha ya Kiingereza, ujuzi wa kompyuta, pamoja na vyeti vya masomo ya Qur'an, hali inayomwezesha kuwasiliana na kufundisha katika mazingira na makundi tofauti ya kijamii.

Katika nyanja ya kazi, Sheikh Hassan amehudumu kama mwalimu wa masomo ya Kiislamu katika taasisi mbalimbali, zikiwemo Albushara Islamic Institute, Ibn Masoud Islamic Center na Ansaar Muslim Youth Center – Ibn Umar Institute, ambako amekuwa akifundisha tangu mwaka 2014 hadi sasa. Kupitia Kongamano la Misk ya Roho, Sheikh Hassan anatarajiwa kuchangia mjadala wa kielimu na kiroho kwa kuwasilisha mada itakayoolenga kuimarisha uelewa wa Qur'an, maadili na nafasi ya elimu ya dini katika kujenga jamii yenye amani na mshikamano.

Misk ya Roho: Ilipoanzia hadi sasa

Kongamano la Misk ya Roho ni jukwaa la da'wah la Afrika Mashariki linaloandaliwa na taasisi ya The Islamic Foundation, likilenga kufikisha ujumbe wa Kiislamu kwa lugha ya Kiswahili. Kongamano hilo lilianza mwaka 2017 baada ya wadau wa da'wah kupendekeza kuwepo kwa jukwaa la kimataifa la Kiswahili, kufuatia changamoto ya lugha katika makongamano makubwa ya awali.

Baada ya kufanyika kwa mafanikio makubwa katika miaka yake mitatu ya mwanzo, kongamano hilo lilisimama kwa kipindi cha miaka mitano kutokana na changamoto za kifedha na athari za janga la Corona. Hata hivyo, kwa mujibu wa waandaaji, kiu ya jamii ya kuliona likirejea iliendelea kuwepo, hali iliyopelekea maamuzi ya kulirudisha tena mwaka huu.

Kwa mwaka huu, kongamano linatarajiwa kufanyika Desemba 27 katika Ukumbi wa Diamond Jubilee, Dar es Salaam, likiwa na kauli mbiu inayojikita katika amani na mshikamano wa jamii. Waandaaji wanasema Misk ya Roho si tu jukwaa la kusikiliza mihadhara, bali pia ni fursa ya kujenga mtandao wa mahusiano, kubadilishana uzoefu na kuimarisha umoja wa Waislamu wa Afrika Mashariki.

Sheikh Twalib Hassan Ghalib *wa Uganda*

Sheikh mwingine ni Twalib Hassan Ghalib wa Uganda ambaye pia ni miongoni mwa masheikh vijana wa ukanda huu wa Afrika ya Mashariki lakini waliobobea katka da'awah.

Misk ya Roho
MWAKA 1447H/2025

Kongamano La 4 La Afrika Mashariki

The Islamic Foundation

VITUO VYA TIKETI

1 ABDULRASHID SAID 0692 600 289

Wakazi wa Homboza, Chanika yote, Mongo la ndege, Kivule na maeneo ya jirani wafike Masjid Lijumaa Gongo la Mboto

2 AHMAD UYAI (KINDEGE) 0717 081 199

Wakazi wa Mikwambe, Kibada Kisarawe Tu, Mji Mwema, na Geza Ulole Vijibweni na maeneo ya jirani wafike Kigamboni Fery

3 KANZU POINT 0744 577 577

Wakazi Kariakoo Mnazi Mmoja, Jangwani, Gerezani na maeneo ya jirani fika city mall barabara ya Morogoro na bibi titi.

4 USTADH MUSTAFA SALIM 0787 620 235

Wakazi Wa Temeke, Mtoni, Mtongani, Buza, na maeneo ya jirani wafike Tandika Masjid Irshaad Chihota

5 MKOMELA A MKOMELA 0784 328 512

Wakazi wa Kisewe, Mbande, Chamazi, Kongowe, na Vikindu wafike Mbagala Rangi Tatu, Sokoni

6 WAZIRI SONYO 0714 541 957

Wakazi Wa Manzese, Mburahati, na maeneo ya jirani wafike Masjid Kichangani Magomeni

7 PEACE TRAVEL 0763 323 232

Mkabala na msikiti wa Manyema Dar es Salaam

8 TASTE ME DESERTS AND CAFE 0757 446 444

Iliopo Coco beach

9 DISCOUNT CENTRE 0759 130 000

Mwenge Natai plaza

10 TASTE ME MART 0765 333 633

Iliopo Upanga

11 RAJABU FARIJALA AMIR WA UMASATA 0784 827 337 na 0715 827 337

Kwa mahitaji ya kuletewa tiketi popote ulipo

27 Disemba | 2:00 Asubuhi - 11:00 Jioni | Diamond Jubilee - Dar Es Salaam

"Muhammad ﷺ Msingi wa Amani"

MEDIA PARTNER'S 2025
azam media · azam tv · ZBC2 · DUA tv · AL-HAAJAR TV · tv Imaan Tanzania · Radio Imaan FM · IMAAN NEWSPAPER · IMAAN DIGITAL

Mwinyi: Tuendelee kuiombea nchi amani na utulivu

Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Ali Mwinyi amesema hakuna mbadala wa amani, hivyo amewahimiza Waumini wa Dini ya Kiislamu na Watanzania kwa ujumla kuendelea kuilinda na kuikuza amani.

Dkt. Mwinyi ameyasema hayo Disemba 12, 2025 alipojumuika na Waumini wa Dini ya Kiislamu katika ibada ya sala ya Ijumaa katika msikiti wa Muhammad uliopo Mwanakwerekwe, Mkoa wa Mjini Magharibi.

Katika mazungumzo yake, Rais Dkt. Mwinyi amesema nchi isiyo na amani haiwezi kutekeleza shughuli zozote za maendeleo na kuwasisitiza viongozi wa dini kuendelea kuhubiri amani ili Taifa liweze kusonga mbele kimaendeleo.

Akizungumzia suala la urafiki ambalo lilikuwa mada kuu katika hotuba ya Ijumaa, Rais Mwinyi amesema kuna umuhimu mkubwa kwa vijana kuchagua marafiki wenye maadili mema, huku akiwahimiza wazazi kufuatilia mienendo ya vijana wao ili kuwaepusha na marafiki wasiofaa.

Ameongeza kuwa kwa sasa kuna njia nyingi za kupata marafiki ikiwemo kupitia mitandao ya kijamii, hivyo amewataka vijana kutafakari kwa kina na kuchagua marafiki wema wenye maadili yanayokubalika katika jamii.

> “Sasa kuna njia nyingi za kupata marafiki ikiwemo kupitia mitandao ya kijamii, hivyo vijana watafakari kwa kina na kuchagua marafiki wema wenye maadili yanayokubalika katika jamii
>
> **Rais Dkt. Hussein Ali Mwinyi**

Bei za petroli, dizeli zashuka Zanzibar

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (Zura), imetangaza kushuka kwa bei za mafuta huku mafuta ya taa yakisalia kwenye bei yake.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotumwa kwa vyombo vya habari jana na kuthibitishwa na Meneja wa kitengo cha uhusiano Zura, Mbaraka Hassan Haji, bei hizo zilianza kutumika rasmi jana.

Alisema, kwa mwezi huu (Desemba) lita moja ya petroli itauzwa kwa Sh2,815 kutoka Sh2,868 ya mwezi uliopita (Novemba) sawa na punguzo la Sh53.

Pia, bei ya dizeli itakuwa Sh2,944 kutoka Sh3,004 ya Novemba sawa na punguzo la Sh60 na bei ya mafuta ya taa imesalia kwenye bei ya Sh3,000 kama ilivyokuwa Novemba.

جمادى ثاني

HABARI
DAR ES SALAAM

MWANDISHI WETU

Uhaba wa maji wakumba mikoa sita

Mwonekano wa sehemu ya Mto Ruvu ambao maji yamepungua kwa kiasi kikubwa kutokana na upungufu wa mvua na kusababisha upungufu maji katika mikoa ya Pwani na Dar es Salaam.

Wakazi wa mikoa ya Dar es Salaam, Simiyu, Pwani, Morogoro, Dodoma na Arusha wanakabiliwa na uhaba mkubwa wa maji, unaotajwa kuwa miongoni mwa mikubwa zaidi katika miaka ya karibuni, hali inayozilazimu kaya na biashara kuchukua hatua kali ili kuendeleza maisha ya kila siku.

Jijini Dar es Salaam, familia zimeanza kununua maji ya chupa kwa ajili ya kupika, kusitisha shughuli zinazohitaji maji mengi, kuhifadhi kila tone linalopatikana kwenye ndoo na mapipa, pamoja na kutegemea kwa kiasi kikubwa visima binafsi. Uhaba huo umebadilisha kabisa ratiba za maisha, huku wakazi wengi sasa wakipanga shughuli za nyumbani kulingana na upatikanaji wa maji usiotabirika.

Dumu la lita 20 la maji jijini humo linauzwa kati ya Sh1,500 na Sh2,000—bei ambazo kaya nyingi zenye kipato cha chini haziwezi kuhimili kwa muda mrefu. Morogoro hali ni mbaya zaidi, ambapo baadhi ya jamii zimeanza kutumia maji machafu yanayotoka bondeni na mito ya msimu, hali inayozua hofu ya hatari za kiafya.

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (Dawasa) imesema uzalishaji wa maji katika Kituo cha Kutibu Maji cha Ruvu Chini umeshuka kwa kiasi kikubwa kutoka lita milioni 270 kwa siku hadi takribani lita milioni 50, hali iliyopunguza kwa kiasi kikubwa usambazaji wa maji jijini Dar es Salaam na maeneo ya jirani.

Mamlaka hiyo imeeleza kuwa kushuka huko kunatokana na kupungua kwa kina cha maji katika Mto Ruvu, sambamba na hali ya ukame iliyodumu kwa muda mrefu. Mapema mwezi huu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) ilieleza kuwa upungufu wa mvua unatokana na athari za La Niña, hali inayotarajiwa kupungua ifikapo Januari. Aidha, nchi inakumbwa na ongezeko lisilo la kawaida la joto. Novemba 21, Moshi mkoani Kilimanjaro ilirekodi nyuzi joto 35.7°C, takribani nyuzi 4.2 juu ya wastani wa muda mrefu, hali inayoongeza uvukizaji wa maji na mahitaji yake.

Katika maeneo ya Dar es Salaam kama Goba, Mbezi na Tabata, wakazi wanasema maji yanapatikana mara chache au hayapatikani kabisa. Mkazi wa Goba, Bi Rose Joseph, alisema familia yake huweka ndoo tayari wakati wote lakini mara nyingi huishia kununua maji endapo ratiba ya usambazaji itashindikana. “Wakati mwingine tunanunua chombo cha lita sita kwa Sh4,000 kwa ajili ya kupika tu. Hata maji ya bomba yenye chumvi yakipatikana, foleni huwa ndefu kiasi kwamba tunaweza kusubiri kwa siku kadhaa,” alisema.

Vivyo hivyo, Bi Rehema Rajab wa Kimara Suka alisema eneo lao limekaa karibu wiki tatu bila maji ya bomba. Kaya sasa zinategemea visima virefu binafsi, ambako ndoo moja inauzwa Sh300 au zaidi. “Kwa kupika hatuna mbadala. Maji ya chupa ni muhimu kwa sababu maji yenye chumvi hayafai,” alieleza.

Katika eneo la Magarisaba, mwenye nyumba Bw Goodliving Emmanuel alisema amewashauri wapangaji kusitisha kwa muda shughuli zinazotumia maji mengi kama kufua nguo ili kuhifadhi maji machache yanayopatikana. “Wameelewa hali ilivyo, na wengi wanatumia maji yenye chumvi kutoka kwenye visima binafsi kwa mahitaji ya msingi,” alisema.

MUGINI SINGIRA

Serikali yaipongeza Saudi Arabia kufadhili masomo kwa Watanzania

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda amekutana na kufanya mazungumzo na Balozi wa Saudi Arabia hapa nchini, Yahya Bin Ahmed Okeish kuhusu kuimarisha sekta ya elimu na kupanua fursa za ufadhili wa masomo kwa vijana wa Kitanzania.

Mazungumzo hayo kati ya Waziri Mkenda na Balozi Okeish yamefanyika Disemba 11, 2025 jijini Dar es Salaam, ambapo Waziri Mkenda ameishukuru na kuipongeza Serikali ya Saudi Arabia kwa kuongeza nafasi za ufadhili wa masomo ya elimu ya juu kutoka 90 hadi 127 kwa Watanzania.

Kupitia mkutano huo, Waziri Mkenda amesema Serikali itaendelea kuhakikisha fursa hizo zinatumika kikamilifu ili kuwawezesha vijana kupata elimu bora katika vyuo na taasisi mbalimbali nchini Saudi Arabia.

Amesisitiza kuwa Serikali ya Tanzania inaendelea kuimarisha mfumo wa elimu kupitia maboresho ya kimkakati katika nyanja za sayansi, teknolojia, uhandisi, sayansi ya takwimu na akili unde ili kuwajengea vijana ujuzi unaoendana na mahitaji ya soko la ajira ndani na nje ya nchi.

Kwa upande wake, Balozi Okeish amesema kuwa Saudi Arabia inajivunia uhusiano wake na Tanzania katika kukuza elimu na kuahidi kuendeleza ushirikiano huo kwa kuunga mkono mikakati ya kukuza ujuzi wa vijana wa Kitanzania, hususan kwenye maeneo yenye vipaumbele vya kitaifa. Aidha, Balozi huyo ameipongeza Wizara ya Elimu kwa kuwa na sera bora ya elimu, ambapo amewakaribisha viongozi wa Tanzania kufanya ziara nchini Saudi Arabia kutembelea vyuo mbalimbali kwa ajili ya kubadilishana uzoefu na kupanua fursa za elimu kwa vijana wa mataifa hayo mawili. Pia ameahidi kuunga mkono mpango wa kuimarisha ufundishaji wa lugha ya Kiarabu hapa nchini.

MAKALA MAALUM

SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

Tujifunze kutoka historia athari za vurugu za kisiasa

Tarehe 29 Oktoba 2025 imebaki kama kumbukumbu yenye mafunzo makubwa kwa taifa letu. Vurugu zilizojitokeza katika maeneo mbalimbali nchini zilichochewa na sintofahamu, chuki za kijamii, na misuguano ya kisiasa.

Matukio yale yalituonesha jinsi machafuko ya umma yanavyoweza kuigeuza hali ya kawaida ya utulivu kuwa mazingira ya hatari yasiyotabirika na kuweka rehani maisha ya watu - wenye hatia na wasio na hatia - kupelekea baadhi kupata ulemavu na kuhatarisha usalama wa mali zao.

Vurugu hizo zilizojumuisha uporaji, uharibifu na uchomaji wa mali za thamani za wananchi na miundombinu muhimu ya taifa ikiwemo mabasi ya mwendokasi, magari ya Serikali, na hata vituo vidogo vya polisi (polisi posti) zilizaa hofu na kuteteresha misingi ya ustawi wa taifa.

Athari ya vurugu zile ni nyingi ikiwemo kupungua kwa ushirikiano wa kijamii, kuongezeka kwa hofu na sintofahamu, na kuibuka kwa hali ya kutoaminiana miongoni mwa raia. Mambo yasiposhughulikiwa yatadhoofisha zaidi umoja wa kitaifa na kuzorota kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Ni hatari zaidi vurugu za aina ile zikihusisha makundi ya kidini au kikabila. Katika mazingira ambayo mivutano ya kijamii inachanganyika na tofauti za kiimani na kimaslahi, mgawanyiko hukua kwa kasi, chuki hujengeka, na hatimaye matokeo huwa mabaya zaidi.

Katika haya, historia inatukumbusha kwa mifano mingi isiyokuwa na huruma.

Mifano ya vurugu iliyovuruga nchi

Kule Haiti mwaka 2019, machafuko ya mtaani yalizua wimbi la uchomaji moto maduka, uporaji wa mali binafsi na za Serikali, na kuathiri vibaya uchumi wa wananchi wa kawaida. Huduma za msingi zilisambaratika, na maisha ya raia yakawa katika hatari ya kudumu.

Kwa upande wa Zimbabwe, mwaka 2008, migogoro ya kisiasa ilisababisha maandamano yaliyogeuka kuwa vurugu, kuharibu biashara na mali za watu binafsi huku miundombinu ya umma ikiporomoka. Taifa liliachwa kwenye hali tete ya kiuchumi na kijamii.

Nako kule Nigeria, mwanzoni mwa miaka ya 2010, sintofahamu za kijamii na kisiasa zilichochea kuongezeka kwa mirindimo ya mabomu ya kigaidi, mauaji ya raia wasio na hatia, utekaji, kujiteka, uchomaji wa miundombinu, na uharibifu mkubwa wa mali za umma na binafsi. Hofu, chuki ya kidini, na mgawanyiko wa kijamii viliongezeka kwa kasi.

Libya ni mfano mwingine halisi wa namna sintofahamu za kisiasa zinavyoweza kuvuruga taifa. Machafuko yalianza mwaka 2011 baada ya maandamano dhidi ya utawala wa Kanali Muammar Gaddafi na baadaye kugeuka vita kati ya waasi na Serikali. Kuanguka kwa utawala kulisababisha pengo la uongozi ambalo liliachwa wazi na taasisi dhaifu.

Matokeo yake, makundi ya kikabila na kijeshi yalishindania madaraka na rasilimali za mafuta, na taifa likajikuta likiwa na Serikali mbili hasimu. Uharibifu wa miji, biashara, miundombinu, na maisha ya raia ulifikia viwango vya kutisha, na mpaka leo taifa linaendelea kulipa gharama ya mgawanyiko huo.

Kwa upande wa Sudan, baada ya kuondolewa kwa Omar al-Bashir mwaka 2019, taifa hilo liliingia kwenye kipindi cha mpito kilichohitaji umoja na uongozi madhubuti. Badala yake, makundi mawili ya kijeshi—jeshi la Sudan (SAF) na kikosi cha Rapid Support Forces (RSF)—yalitofautiana kuhusu nani anapaswa kuongoza taifa.

Mivutano hiyo huko Sudan ilisababisha vita vya mwaka 2023 vilivyoleta maelfu ya vifo, maelfu kupoteza makazi, uharibifu wa hospitali, shule, na biashara. Uchumi ulianguka, na raia wa kawaida wakawa waathirika wakuu wa mzozo huo.

Kila tukio kama hili linatukumbusha kwamba vurugu haziharibu mali tu, bali huweka rehani mustakabali wa taifa lote. Zinaangamiza rasilimali, kuua watu wasio na hatia, kuporomosha uchumi, na kumomonyoa mshikamano wa kijamii. Amani inapopotea, ujenzi wa taasisi, maendeleo ya kiuchumi, na ustawi wa wananchi hubaki kuwa ndoto isiyoweza kutimia.

Matukio ya hivi karibuni nchini mwetu yametukumbusha kwamba tunapopuuza thamani ya tunu ya amani, rasilimali zilizojengwa kwa miaka mingi kwa nguvu, jasho, na rasilimali zinaweza kuharibika ndani ya muda mfupi sana.

Hadi vurugu kutawala, inaweza kuwa zimewsababishwa na vyanzo vingi visivyokuwa rahisi kuvidhibiti, na matokeo yake ni kupotea kwa maisha ya wengi, uharibifu wa mali, na kuyumba kwa utulivu wa taifa.

Ni wajibu wa kila mwananchi kutambua nafasi yake katika kulinda amani. Lazima tujifunze kuheshimiana, kulinda mali za wengine, kuthamini maisha, na kushirikiana kukabiliana na changamoto zetu bila kutumia nguvu. Tunapaswa kukuza utamaduni wa ustahimilivu, mazungumzo, na maridhiano badala ya kutafuta mchawi. Hakuna maendeleo ya kweli yanayoweza kupatikana katika mazingira ya vurugu, ugaidi, uchomaji moto, uporaji, utekaji, kujiteka au uharibifu wa mali. Amani ni nyenzo ya msingi inayolinda usalama wa kila mmoja wetu na mustakabali wa taifa.

MAKALA MAALUM

SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

Nasaha juu ya kupokea maumivu ya kukosa uteuzi

Katika kila msimu wa uchaguzi, huwa kuna mashujaa wengi wasiojulikana. Watu wanaotumia jasho, muda, rasilimali na hata heshima binafsi ili kusukuma gurudumu la mabadiliko ya kisiasa.

Katika kampeni, kwenye mitandao ya kijamii na kwenye vijiwe vya hoja, wapo waliopigana hadi mwisho kwa matumaini kwamba ushindi utaleta neema si kwao tu, bali kwa Taifa zima.

Lakini baada ya ushindi, sura halisi ya siasa hujitokeza. Majina yanapotangazwa, magari ya viongozi yakikatiza barabara kuelekea Ikulu au ofisi mpya, kuna watu wengi wanaotazama tukio hilo kupitia madirisha yao, wakivuta pumzi ndefu na kujiambia kimoyomoyo: "Nilipambana pia… lakini inaonekana zamu yangu haikuwa leo."

Hawa ndio watu wanaobaki na sintofahamu nzito. Waliopigana kwenye mstari wa mbele, lakini sasa wako nje ya duara la uongozi. Ni kana kwamba mchango wao ulionekana wakati ule wa mapambano tu, si wakati wa ushindi.

Chukua mfano wa kijana aliyetembea takriban vijiji zaidi ya 300 akihamasisha wananchi. Mara nyingi alitumia wakati na pesa yake binafsi. Marafiki wanampa moyo: "Safari hii lazima upewe nafasi angalaa Mkuu wa Wilaya." Lakini majina ya wateule yanasomwa, yeye hayupo. Hakupokea simu ya uteuzi. Wala shukurani rasmi. Hakuna chochote kinachodhihirisha kuthaminiwa kwa mchango wake. Pasina shaka simulizi kama hii imezagaa kote nchini.

Nafasi chache, wengi wanaostahili

Wachambuzi wa siasa wanakiri kuwa kutoteuliwa katioka nafasi za kiuongozi sio dalili ya kutothaminiwa juhudi za mtu kwani idadi ya watu wanaojitolea ni kubwa mno kuliko nafasi zilizopo.

Kwa uzoefu, zaidi ya asilimia 90 ya wapiganaji hubaki nje ya mfumo si kwa sababu hawakustahiki, bali kwa sababu mfumo hauwezi kuwakumbatia wote.

Takwimu zinathibitisha hili wazi: Tanzania ina zaidi ya watu milioni 60. Mawaziri ni chini ya 40. Wakuu wa mikoa bara na visiwani si zaidi ya 31. Wakuu wa wilaya ni 139. Mabalozi ni wachache zaidi. Kama kila aliyejitolea

Qur'an inasema: "Huenda mkachukia jambo lolote lile, na kumbe Allah ameweka kheri nyingi ndani yake." [Qur'an, 4:19]. Huenda kutoteuliwa kumemlinda mtu na hatari asiyoijua.

kukipambania chama chochote kile kwenye kipindi cha kampeni angepewa cheo, basi Serikali ingebidi kuwa na wizara kama makundi ya WhatsApp.

Uhalisia ni kwamba sio kila mchango uliooutoa unalipwa kwa cheo, na siasa huwa haifuati hesabu ya "nilitoa hiki, napewa kile".

Hisia za aliyekosa cheo

Kwa mtu ambaye aliamini kwa dhati kuwa na yeye ataonwa, kukosa nafasi humuumiza sana. Kutoteuliwa hupelekea mtu kukata tamaa, kuhisi jitihada zake zimepuuzwa na ametumiwa, akihisi walinikumbuka wakati wa vita, si wakati wa ushindi.

Hali hii pia hupelekea husda za kisiasa hasa akiona waliojitokeza dakika ya mwisho ndio walioteuliwa. Anajiuliza, alipungukiwa wapi, huku pia akipata shinikizo la jamii kumzodoa: "Kiko wapi?" au "Mbona wewe hujapewa kitu?"

Taswira inayogusa moyo

Fikiria hii: Barabara ya kuelekea Ikulu imepambwa kwa bendera, magari ya viongozi yanapita yakipiga ving'ora vya furaha. Wakati huo huo, kwenye kijumba chako pale Shimo la udongo, unatafakari namna ulivyokipambania chama chako. Hakuna anayekukumbuka ilhali wewe ndiye uliyewashawishi mamia ya wapiga kura.

Hapo unagundua kuwa siasa ni mavuno ya wachache kutokana na juhudi za wengi: Hawa wachache si bora kuliko wengine, wakati mwingine ni suala la qadar, muda, nafasi, bahati, mazingira, au mkondo wa historia.

Siasa haina daftari la 'mnapewa wote'. Haina mzazi anayeweka foleni ya haki sawa. Kuna siku unatoa, siku nyingine unangoja, siku nyingine unapata, na siku nyingine unapoteza au hupati kabisa.

Nasaha kwa Muislamu aliyekosa cheo

Kwa Muislamu, suala la kukosa cheo lina mwanga mzito wa kiimani.

Mosi, cheo ni mtihani, sio zawadi: Hadith sahihi inasema: "Usiombe uongozi… ukipewa bila kuutafuta utasaidiwa, lakini ukiutafuta mwenyewe utakabidhiwa bila kusaidiwa." [Bukhari & Muslim]. Hii inafundisha kuwa kutopewa cheo ni rehema, na kukipata ni mzigo.

Pili, Allah ndiye humpa mtu mamlaka: Allah anasema: "Utukufu wote ni wa Allah. Humpa amtakaye." [Qur'an, 3:26]. Aya hii inamtoa mtu kwenye presha ya "nilistahili".

Tatu, kheri ya Allah hujificha mahali usipotarajia

Qur'an inasema: "Huenda mkachukia jambo lolote lile, na kumbe Allah ameweka kheri nyingi ndani yake." [Qur'an, 4:19]. Huenda kutoteuliwa kumemlinda mtu na hatari asiyoijua.

Nne, subira, msingi wa mafanikio. Allah anasema: "Na subirini; hakika Allah yuko pamoja na wenye subira." [Qur'an, 8:46].

Siku ya mtu huja tu. Wengine hupata baada ya miaka mingi. Wengine hupata bila hata kutegemea.

Tano, kazi ya mtu haipotei kwa Allah: Allah anasema: "Na Allah hapotezi malipo ya watendao mema." [9:120]. Unaweza ukakosa cheo, lakini thawabu zako haipotei.

Kwa hiyo, kama ulipambana lakini hakuona jina lako kwenye orodha ya uteuzi, dumu katika uzalendo, endelea kuchapa kazi ukielewa kuwa safari ya uongozi ina zamu, na utafika muda wako wa kupokea kijiti.

Mwandishi ni Katibu wa Baraza la Kuu la Jumuiya za Ansaar Sunna Tanzania (BASUTA).

HUDUMA ZA KIFEDHA ZA KIISLAMU

Uganda yazindua bima ya Takaful

Uganda imeandika historia mpya katika sekta ya bima baada ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bima (Insurance Regulatory Authority – IRA) kuzindua rasmi kanuni za bima ya Takaful na Re-Takaful, hatua inayofungua mlango kwa mara ya kwanza kwa huduma za bima zinazozingatia Sheria ya Kiislamu (Shari'ah-compliant).

Kanuni hizo mpya zinaanzisha rasmi mfumo wa bima ya Kiislamu (Takaful) nchini Uganda, zikilenga kuwajumuisha mamilioni ya wananchi ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakijitenga na bima za kawaida kutokana na sababu za kidini au kimaadili, hususan marufuku ya riba, kamari na kutokuwa na uwazi.

Kwa mujibu wa IRA, Takaful inajengwa juu ya misingi ya mshikamano, kusaidiana na kugawana hatari, tofauti na bima za kawaida zinazotegemea faida kwa misingi ya riba. Mfumo huu unaruhusu wanachama kuchangia katika mfuko wa pamoja unaotumika kusaidia waliopatwa na majanga, huku uendeshaji wake ukisimamiwa kwa kufuata kanuni za Sharia.

Uganda kuanzisha Takaful kuinaifanya ijiunge na nchi za Afrika zinazojipanga kunufaika na sekta hii inayokua kwa kasi duniani. Takwimu zinaonesha kuwa soko la kimataifa la Takaful lina thamani ya zaidi ya dola bilioni 36, na linatarajiwa kuongezeka maradufu ifikapo mwaka 2033, kutokana na ongezeko la mahitaji ya huduma za kifedha zinazozingatia maadili na ujumuishaji wa kifedha.

Wataalamu wa bima nchini Uganda wanasema kanuni hizo mpya zitasaidia kupanua wigo wa soko la bima, hasa miongoni mwa jamii ambazo awali zilikuwa hazishiriki kikamilifu katika mifumo ya bima. Aidha, hatua hiyo inatarajiwa kuvutia wawekezaji wa ndani na wa kimataifa wanaotaka kuwekeza katika bidhaa za bima zinazozingatia Sharia.

Kwa kuanzisha mfumo huu, Uganda inalenga kuimarisha ujumuishaji wa kifedha, kuongeza ulinzi wa kijamii, na kupanua mchango wa sekta ya bima katika uchumi wa taifa. Hatua hiyo pia inaonesha dhamira ya serikali kuunda mazingira jumuishi ya kifedha yanayoheshimu tofauti za kidini na kimaadili za wananchi wake.

MAKALA MAALUM

Abaid Othman

Haitoshi ujenzi wa vitu, tujenga nafsi adilifu

Katika dunia ya leo, mataifa mengi, yamejikita kwa nguvu kubwa katika ujenzi wa miundombinu kama vile barabara pana, madaraja ya kisasa, hospitali, shule mpya na majengo ya huduma za umma.

Bila shaka, haya ni maendeleo yanayoonekana kwa macho na tunayoweza kujivunia. Lakini tukitafakari kwa mtazamo wa Kiislamu, tunakumbushwa jambo la msingi kuwa maendeleo ya vitu hayawezi kuwa na thamani ikiwa hayaendi sambamba na maendeleo ya nyoyo za watu.

Uislamu unawataka Waumini wajenge dunia kwa juhudi na maarifa, lakini pia unasisitiza sana juu ya kujenga nafsi zenye maadili mema. Mwenyezi Mungu anasema katika Qur'an: "Hakika Mwenyezi Mungu habadili hali ya watu mpaka wabadili yaliyomo katika nafsi zao." [Qur'an, 13:11].

Aya hii inatukumbusha kuwa msingi wa maendeleo ya kweli huanzia ndani ya mioyo ya watu Kwa kuwa na maadili, uadilifu, uaminifu na hofu ya Mwenyezi Mungu.

Bila ya haya, hata tukijenga miji mikubwa na miundombinu imara, tutabaki kuwa jamii inayoharibu tulichokijenga.

Tukitazama hali yetu, tunaona kwamba mara nyingi barabara mpya zinaharibiwa muda mfupi tu baada ya kujengwa. Taa za barabarani zinaibwa, kingo za madaraja zinabomolewa ili kuuza chuma chakavu, na mabomba ya maji yanachanwa kwa tamaa binafsi.

Hii inaonyesha kwamba tatizo si ukosefu wa vitu, bali ukosefu wa nyoyo zilizojengwa kwa maadili mema. Hapa ndipo maneno ya Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) yanapodhihirika:

Mtume alisema: "Hakika katika mwili kuna kipande cha nyama, kikitengenea hutengenea mwili wote, na kikiharibika huharibika mwili wote. Kipande hicho jua ni moyo." [Bukhari na Muslim]. Mtume anatueleza wazi kwamba moyo ndio kitovu cha mwenendo wa mtu. Ikiwa mioyo ya watu haikujengeka kwa maadili ya Uislamu, basi hatuwezi kutegemea kuwa watalinda mali za umma, hata kama zimetengenezwa kwa ubora wa hali ya juu.

Ujenzi wa nyoyo muhimu

Ujenzi wa vitu bila ujenzi wa nyoyo utatengeneza jamii yenye umbile la uharibifu. Hawa ni watu wanaovunja miundombinu bila woga, wanaohonga, wanaoiba, wanaopuuza sheria na wanaotumia mali za umma kwa maslahi binafsi. Uislamu unawakemea vikali watu wa aina hii.

Allah anasema: "Wala msifanye uharibifu katika ardhi baada ya kuwa imetengenezwa." [Qur'an, 7:56].

Aya hii inaweka wazi kwamba uharibifu wa miundombinu, mazingira au mali yoyote ya umma, ni kitendo cha dhambi kinachokwenda kinyume na mafundisho ya Kiislamu.

Katika historia ya Uislamu, maendeleo yalikuwa na mizani mbili: kujenga vitu na kujenga watu. Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alipofika Madina, hakujenga msikiti tu.

Alijenga pia jamii yenye nidhamu, maadili, hofu ya Mungu, mshikamano na uzalendo. Ndiyo maana Waislamu wa mwanzo waliweza kuendeleza dola kubwa bila kuharibu, bila ufisadi na bila uhalifu. Sisi tunapuuza upande huu wa pili, ndipo hasara inapojitokeza.

Uislamu unataka Waislamu wawe watu wanaolinda haki za wengine na mali za umma kama wanavyolinda mali zao binafsi. Mtume alisema: "Muislamu ni yule ambaye Waislamu wengine wamesalimika kutokana na ulimi wake na mkono wake." [Bukhari].

Ikiwa mtu anaiba taa za barabarani, anaharibu kingo za madaraja, au anachana mabomba ya maji, hawezi kuingia katika sifa hii ya Mtume. Huyu ni mtu ambaye jamii haijasalimika kutokana na mikono yake.

Kwa hiyo, ili taifa lipige hatua za kweli, tunahitaji kufufua misingi ya maadili iliyowekwa na Uislamu. Wanajamii lazima wafundishwe thamani ya uaminifu,kuwajibika kwa taifa, kutunza mali ya umma na kutanabahi kuwa Mwenyezi Mungu anawaona.

Hakika, hatuwezi kutegemea barabara idumu ikiwa mtu anaiangamiza bila woga. Hatutegemei taa za barabarani ziishi ikiwa kuna aliye tayari kuiba kwa tamaa. Na hatuwezi kutarajia maendeleo ya nchi ikiwa nafsi hazijajengwa kuwa na hofu ya Mwenyezi Mungu.

Ujenzi wa nyoyo unaanzia nyumbani. Wazazi wana jukumu la kuwalea watoto kwa maadili ya Kiislamu. Watoto wanaofundishwa kupenda mali ya umma, kuheshimu sheria na kupenda nchi yao, watakuwa watu wazima wanaojenga, si wanaobomoa.

Shuleni, walimu wana jukumu la kupandikiza nidhamu; na katika misikiti, viongozi wa dini wana wajibu wa kukumbusha jamii kuhusu thamani ya maadili.

Serikali nayo inapaswa kuendeleza utamaduni wa uwajibikaji na kuwachukulia hatua wale wanaoharibu miundombinu, kwa kuwa Uislamu unasisitiza kutenda haki bila upendeleo. Allah anasema:

"Enyi mlioamini! Kuweni wasimamizi madhubuti wa uadilifu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu..." (Qur'ani 4:135)

Aya hii inatoa msingi wa kuwajibisha wale wanaovunja sheria, ili jamii ijifunze kuwa kufuata maadili ni sehemu ya ustaarabu.

Hivyo, tunapojenga barabara, tujenge pia watu watakaothamini barabara hizo. Tunapojenga madaraja, tujenge pia maadili ya kuzilinda. Tunapoweka taa za barabarani, tujenge pia nyoyo zisizotamani kuiba.

Maendeleo ya vitu yanaonekana kwa macho, lakini maendeleo ya nyoyo yanaonekana katika utulivu, heshima na ustaarabu wa jamii. Uislamu unatutaka tuunganishe haya mawili.

Kwa hiyo, kama taifa, tukitaka maendeleo ya kudumu, ni lazima tukiri kuwa ujenzi wa vitu hauwezi kutenganishwa na ujenzi wa nyoyo. Vinginevyo, tutajikuta tukijenga vitu kwa gharama kubwa na kisha kuharibiwa na mioyo isiyojengeka kiimani na kimaadili.

rogramu za maendeleo.

Aliongeza kuwa ingawa kiwango cha biashara kati ya mataifa hayo hakijafikia matarajio, makubaliano mapya yaliyokamilishwa na yanayosubiri kutiwa saini yanatarajiwa kufungua milango zaidi ya ushirikiano wa kiuchumi.

Tanzania na Qatar zilianzisha rasmi uhusiano wa kidiplomasia tarehe 13 Desemba 1982, ingawa Qatar haikufungua ubalozi wake wa kudumu nchini mara moja.

Hatimaye, Qatar ilifungua ubalozi wake wa kudumu Dar es Salaam mwaka 2012—hatua iliyotajwa kuwa muhimu katika kuimarisha ushirikiano baina ya mataifa hayo mawili. Kwa upande wa Tanzania, ubalozi wake nchini Qatar ulifunguliwa mwaka 2016.

Hafla ya kuadhimisha Siku ya Taifa ya Qatar ilihudhuriwa na mabalozi, wanadiplomasia, viongozi wa Serikali, wawekezaji na wadau wa maendeleo, ikiwa ni ishara ya kuimarika kwa ushirikiano wa kidiplomasia, kiuchumi na kijamii kati ya Tanzania na Qatar.

جمادى ثان

فتاوى

SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

Hukumu ya kuidanganya kampuni ya bima ya afya

Swali: **Kuna madaktari wakigundua mgonjwa ana bima ya afya au takaful, huongeza gharama za uchunguzi kwa kuagiza kila aina ya vipimo. Je, fedha zinazopatikana kwa njia hiyo ni halali au haramu? Ikumbukwe kuwa bima ya afya ni ya lazima hapa nchini kwetu.**

Jibu: Madaktari wanatakiwa kuwa waaminifu, wakweli na kutokuwa wadanganyifu katika kazi yao. Katika Uislamu hairuhusiwi kumwandikia mgonjwa dawa au vipimo ambavyo havihitajiki, kwa kuwa kufanya hivyo ni udanganyifu uliokatazwa.

Ikiwa hatua hiyo inaleta faida ya kifedha kwa hospitali, kwa mfano, kwa sababu dawa zinanunuliwa humo humo hospitalini au kwa sababu hospitali ndiyo inafanya hivyo vipimo, basi fedha zinazoingia kutokana na udanganyifu huo ni fedha haramu, kwa kuwa zimepatikana kwa njia ya udanganyifu na hila.

Na ikiwa daktari anapata asilimia fulani ya mapato kutokana na vipimo au uchunguzi huo, basi kipato hicho pia ni haramu kwake, kwa sababu amekipata kwa njia ya udanganyifu.

Hakuna tofauti kati ya iwapo mgonjwa ndiye anayelipa gharama hizo kwa fedha taslimu ni mgonjwa au ni kampuni ya bima/takaful, hukumu ni hiyohiyo.

Ni lazima kuwa mkweli na muaminifu kwa kampuni ya bima au takaful na hairuhusiwi kuidanganya, kama ilivyo kwa watu wengine wote.

Cha kusikitisha ni kwamba tabia kama hii imekuwa ya kawaida katika siku hizi za mmomonyoko wa maadili, jambo linaloashiria udhaifu wa dini na kupendelea dunia kuliko Akhera.

Allah Mtukufu anasema: "Enyi mlioamini, Msikhini Mwenyezi." Mungu na Mtume, wala msizikhini amana zenu hali mnajua [Qur'an, 8:27]. Na anasema: "Enyi mlioamini, Msiliane mali kwa batili." [Qur'an, 4: 29]. Naye Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Anayetudanganya si katika sisi." [Muslim].

Mgonjwa anapaswa pia kumnasihi daktari ikiwa atagundua kuwa anaagiza vipimo visivyo vya lazima kwa sababu tu ya uwepo wa bima, kwani dini ni nasaha.

Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

Kutoa ushahidi ajali kwa malipo ya bima

Swali: **Nilishuhudia ajali ya gari barabarani na sasa kampuni ya bima imeniomba nikatoe ushahidi kuhusu kile nilichokiona ili wamlipe fidia aliyepata madhara ambaye alikuwa mwanachama wao anayechangia. Je, kutoa ushahidi katika jambo hili ni haramu kwa sababu bima yenyewe inahusisha riba**

Jibu: Mosi: Bima ya kibiashara (commercial insurance) kwa mujibu wa Uislamu ni haramu katika sura zake zote kwa sababu inajengwa juu ya misingi ya riba na michezo ya kubahatisha (kamari).

Pili: Hakuna tatizo kwako kwenda kutoa ushahidi kuhusu ajali uliyoshuhudia, kwa kuwa ushahidi huo unasaidia kubainisha ukweli wa kilichotokea, kumjua aliyesababisha madhara na aliyeathirika, pamoja na maelezo mengine yanayohusiana na tukio. Ushahidi kama huu unalenga kusimamisha haki na kuondoa dhuluma na uonevu.

Kwa hakika, ni wajibu kutoa ushahidi kama hakuna mashahidi wengine isipokuwa wewe, kwa mujibu wa kauli ya Mwenyezi Mungu: "Wala msifiche ushahidi; na atakayeficha ushahidi, basi moyo wake ni wenye dhambi. Na Mwenyezi Mungu anayajua mnayoyatenda." [Qur'an, 2: 283].

Imam Ibn Qudama (Allah amrehemu) amesema: "Kubeba ushahidi na kuupeleka ni faradhi ya kutosheleza (fardh kifaya), kwa kauli ya Mwenyezi Mungu, 'Wala mashahidi wasikatae wanapoitwa.' Na kauli Yake, 'Wala msifiche ushahidi'. Moyo umetajwa kuwa wenye dhambi kwa kuwa ndiko ushahidi unakopatikana. Ushahidi ni amana, hivyo ni lazima kuitoa kama amana nyingine zote." [rejea 'Al-Mughni' 10/154].

Imam Ibn Qudama pia anabainisha: "Ukikumbana na wito wa kubeba au kutoa ushahidi bila kudhurika, ni lazima kuitikia. Ukikataa bila udhuru, ni dhambi ikiwa hakuna mwingine wa kutoa ushahidi. Lakiini pia, kama ushahidi wako ungekusababishia madhara binafsi, basi si lazima.

La muhimu: Hutoathirika eti kwa sababu kampuni ya bima inahusika katika malipo kwani mkosaji analazimika kulipa fidia, na mwathirika ana haki ya kupata fidia hiyo iwe moja kwa moja kutoka kwa aliyesababisha madhara au kutoka kwa kampuni ya bima iliyojitolea kulipa kwa niaba yake.

Kwa hiyo, ushahidi wako unahusu kuthibitisha haki, kubaini aliye na makosa na aliyeathirika, pamoja na maelezo ya tukio.

Ni wajibu kutoa ushahidi kwa uadilifu bila kumili upande wowote, kama Allah anavyosema: "Enyi mlioamini, Kuweni wasimamizi madhubuti kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, mkitoa ushahidi kwa uadilifu. Wala chuki ya watu isikuchocheeni kutokutenda uadilifu. Fanyeni uadilifu; huo ndio ulio karibu zaidi na uchamungu." [Qur'an, 5: 8].

Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

MUGINI SINGIRA

Zanzibar yataja vipaumbele 6 usimamizi majukumu ya viongozi

Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Ali Mwinyi ametaja vipaumbele sita, vikiwa ni mwongozo wa utekelezaji na usimamizi wa majukumu kwa viongozi wakuu wa Serikali katika taasisi wanazoziongoza.

Dkt. Mwinyi ametaja vipaumbele hivyo katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Naibu Mkurugenzi wa Mawasiliano Ikulu, Raqey Mohamed kwenye ufunguzi wa mafunzo ya awali kwa viongozi wakuu wa Serikali, yaliyofanyika katika Chuo cha IIT Madras kilichopo Bweleo, Mkoa wa Mjini Magharibi.

Dkt. Mwinyi ametaja vipaumbele hivyo kuwa ni kasi ya utekelezaji, uwajibikaji, ufanisi katika utendaji, usimamizi bora wa watumishi, matumizi sahihi ya takwimu katika maamuzi, na kuimarisha matumizi ya teknolojia na mifumo ya kidijiti.

Amesema katika kipindi cha pili cha Serikali ya Awamu ya Nane inahitajika kasi ya utekelezaji, uwajibikaji na usimamizi bora wa majukumu ili kupata matokeo chanya katika kuwahudumia wananchi. "Mafunzo haya yana lengo la kuimarisha usimamizi bora wa utendaji, kuongeza uwajibikaji na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi, hivyo yanapaswa kupewa umuhimu mkubwa," aliongeza kusema.

Dkt. Mwinyi amewataka watendaji wa Serikali kuongeza ufanisi na kasi ya utendaji pamoja na kufanya maamuzi kwa usahihi. "Wakati umefika wa kufanya mageuzi makubwa katika matumizi ya takwimu katika kupanga na kutekeleza mipango ya maendeleo kwa ufanisi katika sekta zote za umma," alisema.

Aidha, Dk Mwinyi amehimiza kukuza uelewa juu ya matumizi ya mifumo ya kidijiti ili kuongeza ufanisi na kupunguza muda wa utekelezaji wa majukumu.

Akizungumzia miradi ya maendeleo, Dkt. Mwinyi ameagiza watendaji wakuu kuwa na ratiba ya ufuatiliaji wa miradi kwa ajili ya utatuzi wa changamoto, akisisitiza kutokuwa na miradi inayosimama bila kupatiwa ufumbuzi.

Pia amewataka viongozi hao kuwa karibu na vyombo vya habari kwa lengo la kufikisha taarifa sahihi kwa umma, kudumisha ushirikiano na wadau wa maendeleo na kutumia mbinu za kujenga uhusiano mzuri wa kimkakati na washirika wa maendeleo ili kuitangaza Zanzibar kimataifa.

HABARI
DAR ES SALAAM

NA, MWAJUMA SALUM, BAGAMOYO

Tudumishe maadili bora ndani ya majumba yetu

Sheikh wa Kata ya Zinga, Sheikh Mukrimu Mwinyikondo, amewataka wazazi na walezi kuwalea watoto katika maadili mema tangu wakiwa wadogo ili kujenga hofu ya Mwenyezi Mungu, kuwatambulisha dini yao na hatimaye kuandaa vizazi bora kwa ajili ya jamii na Taifa kwa ujumla.

Sheikh Mwinyikondo alitoa wito huo alipokuwa mgeni rasmi katika mahafali ya shule ya chekechea ya High Vision Islamic Education Center, iliyopo Mtoro - Zinga, wilaya ya Bagamoyo, mkoa wa Pwani. Alisisitiza kuwa malezi bora huanza nyumbani na yanahitaji mshikamano na umoja kati ya wazazi ili kufanikisha ukuaji wa maadili mema kwa mtoto.

Aliongeza kuwa wazazi wanapaswa kuwalea watoto wema watakaowaombea dua, pamoja na kuwa wasimamizi wazuri wa mali za wazazi wao endapo watatangulia mbele ya haki, kwa kuzitunza, kuzisimamia na kuzitumia kwa njia ya kheri. Aidha, aliitaka jamii kudumisha amani ili kuhakikisha maendeleo endelevu ya Taifa.

Kwa upande wake, mwalimu wa shule hiyo, Harith Shabani, aliwahimiza wazazi kuendeleza maadili mema ambayo watoto wamejifunza ikiwemo uwezo mzuri wa kusoma na kuandika kwa lugha za Kiswahili, Kiingereza na Kiarabu pamoja na kusoma Qur'an.

Hata hivyo, Harith alibainisha kuwa shule hiyo inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa vyumba vya madrasa, na akaomba wahisani na wadau wa elimu kusaidia katika ujenzi wa vyumba zaidi ili kuboresha mazingira ya kujifunzia. Naye Imamu wa Msikiti wa Qiblateen, Sheikh Juma Mwinchumu Mrisho, aliwasisitiza wazazi kuwa mfano bora kwa watoto wao kwa kutekeleza ibada na kufuata maamrisho ya Mwenyezi Mungu.

Alisema mtoto hawezi kuwa na maadili mema iwapo mzazi mwenyewe hatendi mema, na hivyo kuwataka wazazi kuishi kwa mujibu wa Qur'an Tukufu na mafundisho ya Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani).

Wataalamu Sukuk wasaka uwiano mahitaji ya Sharia na soko

Soko la kimataifa la sukuk limeingia katika hatua nyeti huku wadau wa fedha za Kiislamu wakijadiliana namna ya kusawazisha mahitaji ya Sheria ya Kiislamu (Sharia) na uhalisia wa masoko ya kifedha.

Hayo yamebainishwa na Khurram Hilal, Afisa Mtendaji Mkuu wa Idara ya Benki za Kiislamu duniani wa Standard Chartered, wakati wa Wiki ya Fedha ya Abu Dhabi (ADFW) 2025.

Akizungumzia zaidi ya miaka 20 ya maendeleo ya sukuk, na kunukuliwa na tovuti ya finews.com/, Hilal alisema mjadala unaoendelea kuhusu viwango na miundo ya sukuk ni muhimu ili zana hizi za kifedha zikubalike zaidi na wawekezaji wa kawaida bila kuathiri misingi ya Sharia.

Alisisitiza kuwa wanazuoni wa Kiislamu wana matarajio halali yanayopaswa kuheshimiwa, lakini mahitaji ya wawekezaji na changamoto za watoaji wa sukuk haviwezi kupuuzwa.

Moja ya hoja kuu inayojadiliwa ni suala la uhamisho wa umiliki wa mali (title transfer) katika miundo ya sukuk. Kwa mujibu wa Hilal, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) umejitokeza kama kinara katika kushughulikia suala hili.

Benki Kuu ya UAE na Mamlaka ya Juu ya Sharia zimekuwa zikishirikiana kwa karibu na wadau wa sekta kupitia Kamati ya Sukuk ili kupata muafaka kabla ya kukamilisha viwango vipya.

Katika fedha za Kiislamu, sukuk zinapaswa kuwakilisha umiliki halisi wa mali au miradi inayoleta faida, badala ya kuwa deni kama ilivyo kwa hati fungani za kawaida. Hata hivyo, kwa sasa sukuk nyingi duniani hutolewa kwa mfumo wa asset-based, ambapo wawekezaji hupata haki za kiuchumi bila umiliki kamili wa kisheria wa mali husika.

Mjadala huu umechochewa zaidi na mapendekezo ya Shirika la Kimataifa la Uhasibu na Ukaguzi wa Taasisi za Fedha za Kiislamu (AAOIFI), kupitia kifungu cha Sharia mpya (SS62), kinachopendekeza uhamisho kamili wa umiliki wa mali kwa wawekezaji wa sukuk.

Ingawa lengo ni kuongeza ulinganifu wa Sharia, baadhi ya wadau wanaona hatua hiyo inaweza kuongeza ugumu wa kisheria na kupunguza mvuto wa sukuk kwa watoaji.

Kutokana na maoni hayo, mchakato wa kuweka viwango vipya kwa sasa umesitishwa ili kutoa nafasi ya majadiliano zaidi. Hilal alisema lengo ni kupata njia ya kati itakayoboresha ubora wa Sharia bila kuathiri ukuaji wa soko la sukuk, ambalo kwa sasa linakadiriwa kufikia thamani ya dola trilioni moja.

Licha ya mjadala huo, Standard Chartered inaona mustakabali chanya wa fedha za Kiislamu, ikitabiri mali za kifedha zinazozingatia Sharia kufikia dola trilioni 7.5 ifikapo 2028, zikichangiwa na mahitaji ya makampuni, ubunifu wa bidhaa na upanuzi wa masoko, hususan Mashariki ya Kati, Afrika na Asia.

Kujibu changamoto ndio siri ukuaji benki za Kiislamu Nigeria

Baraza Kuu la Sharia nchini Nigeria (Supreme Council for Sharia in Nigeria – SCSN) limesema ukuaji wa kasi wa benki za Kiislamu nchini humo unatokana na uwezo wa mfumo huo kutoa suluhisho la kifedha lisilo na riba na linaloendana na misingi ya Sheria ya Kiislamu (Sharia).

Baraza hilo limenukuliwa na tovuti ya Legit likieleza kuwa benki za Kiislamu zimefanikiwa kujibu mahitaji ya kifedha ya jamii bila kutumia miamala ya riba, ambayo ni haramu kwa mujibu wa Uislamu. Kauli hiyo ilitolewa wakati wa warsha ya siku mbili iliyoandaliwa na Kituo cha Mafunzo ya Qur'an cha Chuo Kikuu cha Bayero, Kano (BUK).

Akizungumza katika warsha hiyo, Rais wa SCSN, Dkt Bashir Aliyu Umar, alisema sekta ya fedha za Kiislamu imekuwa tasnia ya mabilioni ya dola, huku Nigeria ikiwa na benki tano kamili za Kiislamu zinazofanya kazi kikamilifu.

"Fedha za Kiislamu zinakua kwa sababu zinajengwa juu ya misingi ya uthabiti na haki. Waislamu wamekatazwa kisheria kuchukua riba, na mfumo huu unatoa mbadala unaokubalika kwa mujibu wa Sharia," alisema Dk Umar.

Dkt Umar, ambaye pia ni Naibu Mwenyekiti wa Chombo cha Ushauri cha Benki Kuu ya Nigeria (Financial Regulation Advisory Council of Experts (FRACE)—kuhusu fedha za Kiislamu—aliongeza kuwa ukuaji wa haraka wa sekta hiyo unachangiwa na msisitizo wake katika maadili, ushirikiano wa hatari, na usimamizi wa fedha kwa uwajibikaji. Aliwataka masheikj kuwa mstari wa mbele katika kusimamia utekelezaji sahihi wa kanuni za Sharia ndani ya benki, kampuni za bima na kampuni za udalali wa hisa. Alisema mchango wa wanazuoni ni muhimu ili kuhakikisha taasisi zote za kifedha zinaendeshwa kwa kuzingatia kikamilifu misingi ya Uislamu. Mkurugenzi wa Kituo cha Mafunzo ya Qur'an, Profesa Ahmad Murtala, alisema warsha hiyo ililenga kuongeza uelewa wa fiqhi ya Kiislamu katika masuala ya benki za kisasa na udhibiti wa kifedha. Alieleza kuwa huo ni mkutano mkubwa zaidi wa fedha za Kiislamu kuwahi kuandaliwa na kituo chochote kaskazini mwa Nigeria, na kuna mpango wa kuurudia katika maeneo mengine ya nchi.

Huduma zinavyorahishia ibada kwa mamilioni ya Waumini Masjid al-Haram

Msikiti Mtukufu wa Makka unaendelea kutoa huduma jumuishi na za kisasa zinazolenga kurahisisha harakati za mahujaji na Waumini wanaofika kutekeleza ibada zao kila siku, huku mamilioni ya wageni wakipita katika eneo hilo takatifu kwa usalama na utaratibu.

Kuanzia Wumini wanapofika katika milango ya Msikiti, mifumo ya uelekezaji iliyo wazi huanza kufanya kazi mara moja.

Milango ya kuingia imewekewa njia maalum zilizopangwa vizuri, skrini za kidijitali zinazoonesha msongamano wa watu katika kila ghorofa, pamoja na huduma mahsusi kwa watu wenye ulemavu.

Huduma hizo wa walemavu zinajumuisha milango maalum, njia panda, viti vya magurudumu, lifti na ngazi za umeme, zote zikiundwa kuhakikisha mtiririko wa watu unaendelea bila msongamano.

Ili kuonesha juhudi hizi na kuongeza uelewa kwa umma, Wizara ya Hija na Umra kwa kushirikiana na Mamlaka Kuu ya Kusimamia Masuala ya Msikiti Mtukufu na Msikiti wa Mtume, imetoa video inayoonesha kwa undani shughuli za kila siku ndani ya Msikiti Mtukufu.

Video hiyo inaonesha ukubwa wa Msikiti Mtukufu, ambao una eneo la zaidi ya mita za mraba milioni 1.8 na una uwezo wa kuhudumia zaidi ya Waumini milioni 2.5 kwa wakati mmoja. Kusimamia harakati katika eneo hilo kubwa kunahitaji maandalizi ya kudumu na uratibu wa hali ya juu.

Picha za moja kwa moja zinaonesha mahujaji wakielekezwa kutoka milangoni kwenda ndani ya Msikiti kupitia alama za sakafuni na skrini za kidijitali zinazowasaidia kuchagua njia zenye msongamano mdogo. Video hiyo pia inaangazia huduma maalum kwa watu wenye ulemavu, pamoja na matumizi ya lifti na ngazi za umeme zinazowezesha kufikia kwa urahisi ghorofa zote.

Kwa upande wa usafiri wa ndani, Msikiti Mtukufu unatoa huduma za viti vya magurudumu na magari ya umeme kwa ajili ya kutekeleza tawafu na sa'i, huduma ambazo zinaweza kuombwa mtandaoni kupitia jukwaa la mamlaka husika. Aidha, kuna huduma ya bure ya kunyoa nywele baada ya kumaliza sa'i, ambapo vinyozi vinavyohamishika vimewekwa karibu na njia za kutoka ili mahujaji wakamilishe ibada zao bila kuondoka eneo la kati.

Huduma nyingine ni pamoja na vyoo vilivyozunguka Msikiti na mifumo ya usafi wa saa 24, pamoja na vituo vya kuhifadhi mizigo vinavyofanya kazi mchana na usiku, ili Waumini waweze kuabudu bila kubeba mizigo yao.

Wizara ya Hija na Umra pia hutoa huduma za mwongozo kwa saa 24 kupitia kituo cha simu namba 1966, pamoja na miongozo ya kielimu kuhusu Msikiti Mtukufu inayopatikana katika lugha 16, hatua inayowasaidia wageni kupanga ibada zao kwa uelewa na utulivu.

Kwa ujumla, huduma hizi zinaakisi kiwango cha juu cha maandalizi na uangalizi kwa Wageni wa Mwenyezi Mungu, zikilenga kuhakikisha uzoefu salama, wenye utulivu na unaokamilisha ibada kuanzia kuwasili hadi kuondoka.

Kwa msaada wa Saudi Gazette

HABARI KIMATAIFA

MAHMOUD NYAMGUMA

Trump ashambuliwa kila kona kwa kuita Wasomali takataka

Rais wa Marekani, Donald Trump amekosolewa vikali kwa kuwaita wahamiaji wakiwemo Waislamu wa asili ya Somalia "takataka,".

Kauli hizo zinahusishwa na ongezeko la vitisho dhidi ya viongozi wa Kiislamu na jamii za wahamiaji. Picha ya Mbunge Ilhan Omar akiwa na watoto wake nje ya jengo la Bunge la Marekani imechochea mjadala mpana kuhusu usalama wa viongozi wa Kiislamu na heshima ya haki za kiraia.

Kwa mujibu wa vyombo vya usalama, mwanamume mmoja mwenye umri wa miaka 30 kutoka Florida anakabiliwa na kifungo cha hadi miaka sita jela baada ya kukiri kutuma vitisho vya vurugu dhidi ya Mbunge Ilhan Omar kupitia mtandao wa X.

Tukio hilo limetajwa na wachambuzi wa haki za binadamu kama mfano wa madhara ya lugha ya chuki, huku ripoti za mashirika ya kiraia zikionyesha kuwa makosa ya chuki dhidi ya Waislamu yaliongezeka kwa zaidi ya asilimia 30 katika miaka ya hivi karibuni, hasa nyakati za kampeni za kisiasa.

Mbunge Ilhan Omar, ambaye ni Mmarekani wa kwanza mwenye asili ya Somalia na wa kwanza kuvaa hijabu kuchaguliwa Bungeni, ametajwa na wanaharakati wa Kiislamu kama ishara ya mafanikio ya ujumuishaji na demokrasia ya Marekani.

Takwimu rasmi za sensa zinaonyesha kuwa asilimia 58 ya Wasomali wanaoishi Marekani walizaliwa nchini humo, huku asilimia 87 ya waliozaliwa nje wakiwa raia halali, jambo linalopingana na hoja za kuwatenga au kuwadhalilisha kwa misingi ya asili au dini.

Wachambuzi pia wameelekeza macho kwenye mjadala wa rushwa uliotajwa na Trump, wakisema kuwa kuhusisha uhalifu na kundi moja la kikabila au kidini ni upotoshaji wa takwimu.

Ripoti za fedha za umma zinaonyesha kuwa katika kipindi hicho hicho, kesi za udanganyifu wa zaidi ya dola bilioni 1 zilihusisha makundi mbalimbali ya Wamarekani, si jamii moja pekee. Vyombo vya habari vya kati vimetakiwa kutumia hoja tunduizi kuhoji matumizi ya fedha za walipa kodi bila kuchagua misingi ya kikabila.

Kwa upande mwingine, mchango wa Waislamu wa asili ya Somalia umeendelea kuonekana katika majimbo kadhaa, ikiwemo Ohio na Minnesota, ambako wamejenga biashara, misikiti na vituo vya kijamii.

Viongozi kama Munira Yasin Abdullahi, Mbunge wa kwanza Mmarekani mwenye asili ya Somalia na Mwislamu katika Bunge la Ohio, wanatajwa kama vielelezo vya ushiriki wa kiraia unaojenga amani na uwajibikaji, licha ya misimamo yao ya kisiasa inayotetea haki za Wapalestina na jamii zilizo pembezoni.

HABARI KIMATAIFA

MAHMOUD NYAMGUMA

Waislamu walalamikia ubaguzi wa kikatiba wakati Austria ikizuia hijab mashuleni

Bunge la Taifa la Austria limepitisha kwa wingi wa kura sheria inayopiga marufuku wasichana walio chini ya umri wa miaka 14 kuvaa hijab shuleni, hatua iliyozua mjadala mpana kuhusu uhuru wa dini na haki za watoto wa Kiislamu.

Sheria hiyo, inayopiga marufuku vazi la kichwani "kwa mujibu wa sheria za Kiislamu" katika shule zote za umma na binafsi, inatarajiwa kuanza kutekelezwa rasmi mwaka wa masomo 2026/2027.

Kwa mujibu wa serikali ya Austria, takribani wasichana 12,000 wanatarajiwa kuathiriwa moja kwa moja na sheria hiyo, huku adhabu ikijumuisha faini kati ya euro 150 hadi 800. Waziri wa Masuala ya Ujumuishaji, Claudia Plakolm, amedai hijab ni "alama ya ukandamizaji," kauli ambayo wachambuzi wa masuala ya jamii wanaiona kama tafsiri ya upande mmoja inayopuuzia sauti za wasichana wa Kiislamu wanaochagua kuvaa hijabu kwa hiari yao.

Tafiti za kijamii barani Ulaya, ikiwemo utafiti wa European Union Agency for Fundamental Rights (FRA), zinaonesha kuwa zaidi ya asilimia 70 ya wasichana Waislamu waliovaa hijabu hufanya hivyo kwa misingi ya imani binafsi, si kulazimishwa.

Vyama vikuu vya siasa vikiwemo OVP, New Austria and Liberal Party (NEOS) na hata Freedom Party viliunga mkono sheria hiyo, ingawa kwa hoja tofauti. Wakati vyama vya mrengo wa kati vilidai vinawalinda watoto, Freedom Party ilihusisha suala hilo na "uhamiaji mkubwa" na kile ilichokiita "Uislamu wa kisiasa," kauli inayotafsiriwa na wadau wa haki za binadamu kama kuchochea hofu na chuki dhidi ya Uislamu.

Takwimu za Pew Research Center zinaonesha kuwa sera za aina hii huongeza mgawanyiko wa kijamii badala ya ujumuishaji, hasa kwa jamii za wachache wa kidini.

Upinzani pekee ulitoka kwa Chama cha Greens, ambacho kilionya kuwa sheria hiyo inafanana kwa kiwango kikubwa na ile ya mwaka 2019 iliyofutwa na Mahakama ya Katiba mwaka 2020 kwa kukiuka kanuni ya usawa. Naibu Kiongozi wa Bunge, Sigrid Maurer, alisema wazi kuwa serikali "inafahamu sheria hii itaangushwa tena," akisisitiza kuwa hairuhusu usawa kwa watoto wote bila kujali dini zao.

Kwa upande wake, Jumuiya ya Kidini ya Kiislamu Austria (IGGO) imetangaza kuwasilisha rufaa ya haraka Mahakamani, ikieleza kuwa sheria hiyo inaleta "changamoto nzito za kikatiba na haki za binadamu." IGGO imesisitiza kuwa inakataa vikali kulazimishwa kwa watoto, lakini inalazimika kutetea haki za wale wanaochagua hijab kwa hiari. Tayari mawakili na walimu Waislamu wameungana kupinga sheria hiyo, wakidai inakiuka uhuru wa dini uliolindwa kikatiba.

KUTOKA KWA MHARIRI

Msamvu, Morogoro
P.O.Box 6011
Morogoro,
Tanzania

Mhariri
+255 789 201383

Maandalizi muhula wa masomo 2026 yaanze mapema

Aghalabu kila ifikapo mwisho wa mwaka wazazi na walezi huwa na pilikapilika nyingi za maandalizi ya shule kwa ajili ya watoto wao, ikiwamo kulipa ada, kununua sare za shule, madaftari, na kadhalika.

Maandalizi haya ni muhimu mno kwani yatawasaidia watoto kupata elimu itakayowakomboa kifikra na kumudu mazingira yanayowazunguka. Kama ukweli ndiyo huo, ni vizuri kuwaandalia watoto vifaa vya shule mapema kwa ajili ya msimu mpya wa masomo hapo mwezi Januari 2026.

Hii ni kutokana na ukweli kwamba kununua vifaa mapema humjengea mtoto hali ya kujiamini na kuwa na hamu ya kwenda shule na hasa akipata vifaa ambavyo alikuwa anatamani kuwa navyo. Wataalamu wa saikolojia wanatuambia, mtoto huwa na ari na shauku ya kwenda shule ikiwa mzazi/mlezi wake atamnunulia vifaa vipya vya shule ikiwamo nguo, viatu, madaftari na begi.

Ni kweli kwamba wapo baadhi ya wazazi na walezi waliozoea kufanya maandalizi ya vifaa vya shule vya watoto wao kwa zima moto. Kwa mfano, kama shule zinafunguliwa Jumatatu, basi Jumamosi au Jumapili ndiyo huanza kufanya manunuzi ya vifaa mbalimbali vya shule, jambo ambalo huwa gumu pale baadhi ya vifaa vinapoadimika.

Kwa kuzingatia kuwa baadhi ya wafanyabiashara wana desturi ya kupandisha bei za vifaa vya shule mwishoni mwa mwaka, tunashauri wazazi kununua vifaa muhimu mapema kabla bei haijapanda zaidi.

Fauka ya hayo, inapendeza mzazi kumuahidi zawadi mtoto wake endapo atafaulu vizuri masomo yake ili kumjengea shauku ya kupenda shule na ari ya kujituma zaidi katika masomo. Na zawadi bora ni ile inayoendana na hulka na mahitaji ya mtoto.

Pia, ni muhimu kumhimiza mtoto kushikamana na tabia njema, sambamba na kumueleza matarajio yako kwake na kwa namna gani elimu yake itachangia kutimiza ndoto zake na kufikia malengo anayoyatamani.

Tabia njema imesisitizwa katika Uislamu kwa sababu imefungamanishwa na aina zote za ibada, ikiwamo faradhi ya kutafuta elimu. Huwezi kukuta Mwenyezi Mungu ameamrisha ibada fulani isipokuwa ibada hiyo lazima itagusia makusudio ya kufaradhishwa kwake. Ni kwa sababu hiyo, Mtume (rehema za Allah na amani iwe juu yake) akasema: "Zawadi bora ambayo mzazi anaweza kumpa mtoto wake ni tabia njema." [Bayhaqi].

Jambo jingine muhimu katika safari ya maandalizi ya kuelekea msimu wa masomo 2026 ni kuchunguza afya ya mtoto kabla hajaanza masomo ili atakapokuwa shuleni aweze kuyamudu masomo vizuri. Ni muhimu wazazi kwenda hospitali kuwafanyia watoto vipimo (body checkup) hasa wale wanaosoma shule za bweni.

Hii itawahakikishia watoto afya ya akili na mwili na kuwawezesha kuyakabili masomo muda wote watakapokuwa shuleni. Kiujumla mzazi anatakiwa kufanya kila analoona kuwa linagusa elimu ya mtoto wake.

Afya
Pure Drinking water

"Afya"is natural source of sweet drinking water from underground stream which is blended with essential minerals to support and aid perfect metabolism.

WATERCOM LIMITED
P.o. Box 20409, Plot N.4005, Kisarawe11 area Temeke, Dar es Salaam, Tanzania. www.watercomtz.com, Email:info@watercomtz.com

MAKALA MAALUM

0712 690 811

NA SHEIKH SEIF RUGA

Hukumu ya khului na masharti yake katika Uislamu

Msingi wa uhusiano wa ndoa ni mapenzi, huruma na ushirikiano. Hizi ni nguzo tatu imara na msingi wa ndoa dhidi ya changamoto na misukosuko ya maisha. Pamoja na kusisitiza kudumu kwenye ndoa, Uislamu haukupuuza uwezekano wa migongano kutokea baina ya mume na mke, ambapo mara nyingine jitihada zote za kulinda uhusiano huo hushindikana.

Hivyo basi, talaka ikawa ni njia ya mume kuivunja ndoa hiyo. Wakati huo huo, Uislamu haukupuuza mahitaji ya mke pale anapoona haiwezekani kuendelea na maisha ya ndoa. Kama ambavyo mume amepewa haki ya kutoa talaka, vivyo hivyo mke amepewa haki ya kujiondoa kwenye ndoa (khului) anayoichukia akihofia kwamba ataacha kutekeleza mipaka (sharia) ya Allah juu ya haki za mumewe.

Wanazuoni wa sheria ya Kiislamu (Al–Fuqahau) wametofautiana katika kufafanua maana ya neno 'khului' kutokana na jinsi walivyolitazama kisheria. Wapo walioona neno hilo kuwa ni 'Faskh', yaani kuvunjika kwa ndoa moja kwa moja bila talaka kutoka kwa mume.

Wengine wameliona kuwa ni talaka, hivyo wakalifafanua kwa maana inayolingana na talaka. Madhehebu ya Hanafi na Malik, wao wanaona khului ni aina mojawapo ya talaka. Kwa upande wa madhehebu yetu ya Shafi na Hanbali wamesema, khului ili iwe talaka ni sharti isemwe kwa tamko la talaka au kwa nia ya talaka ndipo ihesabike kuwa ni talaka.

Maana ya khului

Neno 'khul'u', kwa lugha ya Kiarabu lina maana ya kujivua katika ndoa. Katika muktadha wa sheria ya Kiislamu, khului ni kuvunjika kwa ndoa kunakoombwa na mke, na mume akaridhia ambapo mke anarudisha mahari au sehemu ya mali aliyopewa kama fidia kwa hukumu ya Kadhi au kwa ridhaa yake ili aachwe.

Hivyo basi, kwa mujibu wa maelezo haya, khului hutokana na maombi ya mke, kwa sababu kitendo cha mume kumuacha mke huitwa talaka. Kadhalika, khului ni lazima iambatane na fidia (malipo), ambayo hutolewa na mke au mtu anayemwakilisha – ima kwa mali yake au kwa mali ya mtu mwingine.

Sheria ya mke kujivua katika ndoa imethibiti katika Qur'an Tukufu pale Mwenyezi Mungu aliposema: "...Wala si halali kwenu kuchukua kitu chochote mlichowapa wake zenu, isipokuwa wote wawili wakihofia ya kwamba hawawezi tena kutimiza mipaka ya Allah. Basi mkihofia hivyo si dhambi kwa wote wawili ikiwa mke atajikomboa kwa kitu (fidia)..." [Qur'an, 2:229].

Kuna nguzo kuu nne za kujivua katika ndoa ambazo ni; kwanza mume awe ameoa kwa ndoa sahihi, pili mke awe bado yumo ndani ya ndoa, tatu khului (kujivua) ifanyike kwa ridhaa yake, na nne yawepo malipo au fidia ambayo mke humlipa mume ili ajivue katika ndoa.

Fidia au malipo ni nguzo kuu katika kukubalika kwa khului, kwani ndiyo inayotoa hukumu zake na kuifanya khului itofautiane na talaka. Bila fidia au malipo, khului haiwi sahihi. Na hakuna kosa mume kuchukua fidia hiyo kwa kuwa kuvunjika kwa ndoa halikua chaguo lake na wala hakufanya kwa hiyari yake.

Imesimuliwa kuwa mke wa Thabit bin Qays (Allah amridhie) alikuja kwa Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) akasema: "Ewe Mtume wa Allah, siwezi kumlaumu Thabit bin Qays kwa tabia wala dini, lakini namchukia na naogopa nisije nikakufuru katika Uislamu."

Mtume akamuuliza: "Je, uko tayari kumrudishia bustani yake (ambayo ndiyo mahari aliyompa)?" Akajibu: "Ndiyo." Mtume akamwambia Thabit: "Kubali bustani yake na muache huru." [Bukhari].

Kutokana na tukio hili, wanazuoni wamekubaliana kuwa iwapo mwanamke hawezi kuvumilia kuishi na mume wake, basi Kadhi au kiongozi wa Waislamu anaweza kumtaka mume amkubalie khului, na hata kumwamuru. Hapo mume na mke watakubaliana juu ya kiasi cha malipo kisha mume atasema: "Nimekuvua kwa malipo ya kadhaa," au maneno yenye maana hayo.

Kwa mujibu wa kauli yenye nguvu ya wanazuoni akiwemo Ibn Abbas (Allah amridhie), khului haizingatiwi kuwa ni talaka hata kama imetolewa kwa tamko la talaka. Kwa mfano, mume akisema kumwambia mkewe "Nimekubali mke wangu ujivue katika ndoa kwa malipo ya kiasi fulani cha mali," au akisema, "Nimevunja ndoa ya mke wangu kwa malipo ya kiasi fulani."

Katika hali hii, mume akifanya khului mara mbili, bado anaweza kumrudia mkewe kwa kufunga ndoa mpya bila kuhesabiwa kuwa ni talaka. Wanazuoni wameshauri kuwa, wakati wa kuandika khului mume asiandike "Talaka kwa malipo ya kiasi fulani" bali aandike "Khului (kujivua kwenye ndoa) kwa malipo ya kiasi fulani."

Sababu ni kwamba, majaji (Kadhi) wengi wa Kiislamu huona kwamba, ikiwa khului itafanywa kwa lafdhi ya talaka, basi inahesabiwa kama talaka, jambo linaloweza kuleta madhara kwa mke hasa ikiwa ni talaka ya mwisho.

Madhehebu yetu ya Shafi yameruhusu mume kuchukua malipo kutoka kwa mkewe iwapo wote wawili wamekubaliana. Malipo hayo yanaweza kuwa sawa na mahari aliyompa, au chini yake, au hata zaidi, lakini ni vizuri yasizidi mahari.

Kadhalika, Imam Shafi (Allah amrehemu) amesema, eda ya mke aliyejivua katika ndoa ni vipindi vya hedhi tatu au miezi mitatu. Lakini Ibn Abbas na Ibn Umar (Allah awaridhie) wamesema, eda yake ni kipindi cha hedhi moja au mwezi mmoja tu; na hii ndiyo kauli sahihi. Jambo lingine la kuzingatia ni kwamba, Khului inaweza kufanywa hata kama mke yupo kwenye hedhi au kinyume chake.

NASAHA ZA WIKI
0787 503 085

NA YUSUFU AMINI

Uislamu unavyolinda haki na kuzuia uovu

Neno haki, kwa tafsiri ya kamusi ya Kiswahili sanifu, lina maana ya jambo/ kitu ambacho mtu anastahiki kuwa nacho. Katika muktadha wa sharia ya Kiislamu, haki ni muunganiko wa sharia na maadili, yenye lengo na madhumuni ya kuilea jamii katika amani, furaha, udugu wa kweli na uhusiano mwema baina ya wanadamu.

Katika Uislamu, haki zimegawika katika makundi makubwa sita, nayo ni; mosi haki za Mwenyezi Mungu Mtukufu, pili haki za nafsi, tatu haki za viumbe na mazingira, nne haki za binadamu kwa ujumla wake, tano haki za raia katika Dola ya Kiislamu, na sita haki za maadui (mateka) katika vita.

Haki hizi zimekuja kutosheleza mahitaji ya watu ya kidini na kidunia. Hukumu za haki hizi zote zinalenga kulinda ustawi wa watu kwa kuwapa yale yenye maslahi na kuwakinga na kila lenye madhara kwao.

Ndani ya amri zote za kisharia kuna maslahi ya kidini na kidunia kwa wanadamu. Kinyume chake, kwenye makatazo (marufuku) yote ya kisharia, ndani yake kuna hasara na madhara kwa mwanadamu. Hivyo basi, mtu anayejitenga na makatazo ya kisharia hunusurika na madhara ya kidunia na Akhera pia.

Ukifanya upembuzi kwenye Qur'an Tukufu na Sunna sahihi za Mtume (rehema za Allah na amani iwe juu yake), utabaini ushahidi mwingi unaoonesha wazi kuwa sharia za Kiislamu zinasimamiwa na falsafa zilizo na manufaa kwa umma na mtu binafsi.

Manufaa hujengwa na mambo mawili, na kila moja hulihitajia jingine, na hakuna hata moja linalojitosheleza. Mambo mawili hayo ni kufanya mazuri na kuacha yaliyo na madhara. Kama ambavyo katika kufanya mazuri kuna manufaa na faida, vilevile katika kuacha madhara kuna faida pia.

Kwa anayefuatilia kwa karibu mambo makubwa na mazito yaliyoletwa na sharia atabaini kuwa, sharia imekuja kwa lengo la kutuhifadhi kwa njia ya kutuletea vyenye manufaa na kutuondoshea vyenye madhara vinavyofahamika kisharia kama misingi mikuu mitano, ambayo ni kuilinda dini, nafsi, akili, kizazi na mali.

Misingi hiyo yote huhifadhiwa kwa njia mbili; kwanza kusimamisha nguzo na kuliimarisha shina lake, na pili kuihifadhi na uharibifu unaoweza kuibuka au unaotarajiwa kujitokeza. Na uhifadhi tunaoumaanisha ni kwa njia ya kuilinda baada ya kuwepo.

Kwa mantiki hiyo, kuondosha uharibifu ni jambo la kisharia; na kamwe hatutaweza kuachana nao kwani maslahi/ufanisi hauwezi kupatikana kwa manufaa pekee. Siyo hivyo tu, inapotokea mgongano kati ya viwili hivyo, basi kuondosha uovu hutangulizwa kuliko kutafuta manufaa.

Hili ni jambo linalodhihiri wazi kwenye kanuni isemayo: "Kuondosha uovu hutangulizwa kuliko kupata manufaa." Jambo hili linaungwa mkono na aya mbalimbali za Qur'an tukufu na hadith za Mtume (rehema za Allah na amani imshukie).

Mtume aliwahi kumwambia mkewe, mama Aisha (Allah amridhie): "Ewe Aisha, lau kama jamaa zako wasingelikuwa wapya (yani wametoka katika ukafiri hivi karibuni), ningeliibomoa Al–Ka'aba na kuifanya kuwa na milango miwili; mlango wa kuingilia watu na wa kutokea."

Al–Hafidh Ibn Hajar amesema: "Hii inatufunza kuwa unaweza kuacha lenye maslahi kwa kuchelea uharibifu, aidha unaweza kuacha kuzuwia uovu kwa kuchelea kutumbukia kwenye uovu maradufu."

Na maslahi yapo aina tatu; kuna maslahi yanayotambuliwa na sharia tukufu, maslahi yaliyofutwa na sharia tukufu, na maslahi yasiyotambuliwa wala kufutwa na sharia. Na hapo ndipo wanazuoni wanapopata fursa ya kufanya Ijtihadi kwa kuihusisha hukumu na jambo, mfano kuwaletea watu maslahi au kuwaondolea uharibifu, au ile iliyokusudiwa na sharia tukufu ya kuhifadhi dini, nafsi, akili, mali na vizazi.

Imethibiti kutoka kwa wema waliopita miongoni mwa Masahaba na Tabiina kuwa, wao walitumia nadharia hii kutoa maamuzi katika baadhi ya kadhia ili kuhifadhi misingi ya kisharia katika kiwango cha dharura, kiwango cha uhitaji, na kiwango cha uboreshaji (urutubishaji).

Tunaposema kiwango cha dharura tuna maana ya maslahi yanayoweza kusitisha maslahi ya watu wengine katika maisha yao ya kidini na kidunia, kwani maisha yanapovurugika maslahi hayo nayo husimama. Watu wa dini za mbinguni na wanadamu wenye busara walikubaliana kwamba, jukumu muhimu zaidi kwa binadamu ni kulinda mambo makuu matano yanayoimarisha mazingira ya binadamu – dini, nafsi, akili, kizazi na mali.

Sharia imekuja na taratibu zinazojitosheleza katika kuhifadhi mahitaji/ dharura hizi tano, na kuhakikisha zinaendelea kuwapo katika jamii, au katika suala la kuimarika, kutoharibika na kutoweka.

Kiwango cha uhitaji ni ile hali ya watu kujirahisishia maisha na kujitatulia dhiki, na ambacho mara nyingi husababisha taabu kwa kukosa mahitaji. Hali ya uhitaji isipoangaliwa vizuri, dhiki na taabu huwakumba watu wote.

Ama kiwango cha uboreshaji (urutubishaji) ni pale maslahi yanapolingana na desturi nzuri, maadili mema, na kujiepusha na hali/ mazingira yasiyopendwa na akili timamu. Na miongoni mwa masharti ya kupata mafanikio ya Akhera ni kutoiminya njia ya kumridhisha Allah Ta'ala.

Tuelewe kuwa wanadamu tumeumbwa ili kuijenga dunia, ambayo ndiyo njia ya kupata mafanikio ya Akhera. Allah anasema: "(Kumbuka) Mola wako Mlezi alipowaambia Malaika: Mimi nitamweka katika ardhi Khalifa..." [Qur'an, 2:30]. Na ukhalifa ni kuijenga dunia na kutekeleza sharia za Allah.

Ukisoma maelezo ya Qur'an na hadith za Mtume kuhusu ardhi utaona kuwa, imejengwa kwa lengo la kuleta furaha na kuondoa uovu. Ni kwa msingi huo Allah Ta'ala akataja madhambi ya waharibifu. "Basi yanayotarajiwa kwenu mkitawala ndiyo mfanye ufisadi katika nchi na kuwatupa jamaa zenu? Hao ndiyo ambao Mwenyezi Mungu amewalaani, akawafanya viziwi, na akawapofua macho yao." [Qur'an, 47:22–23].

جمادى ثاني

SEHEMU YA 1

MUSSA IMANI
SHEHA,
ZANZIBAR
0773 181 494

VISA VYA MITUME NA MASWAHABA

USAMA BIN ZAID

Kipenzi cha Mtume na mtoto wa kipenzi cha Mtume

Miaka saba kabla ya hijra, wakati Mtume (Allah amshushie rehema na amani) akitangaza dini ya Allah huku pia akikabiliana na shida na kero kubwa za Makureish, ilimfikia habari njema ya kuzaliwa mtoto aliyekuja kupewa jina la Usama. Uso wa Mtume ulin'gaa kwa furaha.

Mama wa kijana huyo ni Baraka bint Tha'lab Alhabashiya (Ummu Aymana), mjakazi na mlezi wa Mtume (Allah amshushie rehema na amani), na mke wa swahaba mtukufu Zaid bin Haritha, ambaye ndiye haswa baba wa Usama.

Mara kadhaa, Mtume alisikika akisema: "Ummu Aymana ni mama yangu na katika watu wangu." Kabla ya kuolewa na Zaid, mama huyu aliolewa na Ubeid bin Alharith.

Baba wa Usama, Zaid bin Haritha, ni kipenzi cha Mtume. Asili yake, ni Bi Khadija alimpa mumewe huyu Zaid kama zawadi, naye Mtume akamuacha huru.

Si Mtume pekee aliyefurahi kwa kuzaliwa Usama, bali furaha iliwaenea Maswahaba pia. Naam, wao walifurahishwa na kila lililomfurahisha Mtume.

Mtume alimpenda sana Usama kama alivyompenda mjukuu wake Hassan. Mara fulani alimuweka Usama juu ya paja lake na Hassan juu ya paja jingine na kusema: "Ee Allah mimi nawapenda hawa, basi na wewe wapende."

Sifa zake na ushiriki katika safu za jihad

Alipofika umri wa baleghe, zilijitokeza kwake sifa na vipawa vingi vikiwemo tabia njema, akili pevu, umahiri, ushujaa, hekima, uchamungu na kadhalika.

Wakati Mtume analiandaa jeshi kuelekea vita vya Badri, Usama alijitokeza akiwa na vijana wenzake akiomba naye aende vitani. Alipolikagua jeshi, Mtume (Allah amshushie rehema na amani) aliwarejesha baadhi kwa sababu ya umri wao mdogo.

Usama, akiwa miongoni mwa hao waliorejeshwa, aliondoka huku machozi yakimtoka, analia kwa kuwa hakupata fursa ya kupigana na adui chini ya bendera ya Mtume (Allah amshushie rehema na amani).

Ushiriki katika vita vya Khandaq

Ilipofika siku ya vita vya Khandaq (mwaka wa tano Hijriya), Usama alikuja tena akiwa na wadogo wenzake kadhaa ili Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amruhusu kwenda vitani, basi akawa anajiongeza kimo ili Mtume asijekumrejesha kama ilivyotokea katika vita vya Badr.

Mtume alimuonea huruma na kumruhusu kwenda vitani. Wakati huu Usama alikuwa na umri wa miaka kumi na tano tu. [taz. Suwarun mi hayat swahaba uk.228].

Katika vita vya Hunein na Mu'ta

Katika vita vya Hunein (8 hijriya) Waislamu walikimbia kutokana na shambulizi la kushtukiza lililofanywa na makafiri. Hata hivyo, Usama alikuwa miongoni mwa wachache waliothibiti na kumlinda Mtume, mpaka Allah akashusha utulivu kwa Mtume na Waislamu wakajipanga kimapambano na kuwashinda maadui.

Katika vita vya Mu'ta, Usama alipigana kiushujaa chini ya bendera ya baba yake (Zaid). Katika vita hiyo, alishuhudia kwa macho yake baba yake akiuawa lakini hakutetereka.

Kwa ujasiri mkubwa, Usama aliendeleza mapambano chini ya viongozi Jaafar bin Abi Twalib, Abdullah bin Rawaha na Khalid bin Alwalid. Baada ya vita, Usama alirudi Madina huku akiuacha mwili wa baba yake katika ardhi ya Sham na huku akiwa amempanda farasi wa baba yake.

Itaendelea inshaAllah.

JUNAYNAT ALLY DAMA

Dhibiti sukari ya damu upunguze kwa nusu hatari ya magonjwa ya moyo



Kwa muda mrefu, watu wengi waliogundulika kuwa katika hatua ya mwisho kupata sukari (prediabetes) wamekuwa wakishauriwa kubadilisha mtindo wa maisha kwa kufanya mazoezi zaidi, kupunguza uzito na kula chakula bora ili kujikinga dhidi ya magonjwa ya moyo.

Hata hivyo, utafiti mpya wa kimataifa ulioongozwa na wataalamu kutoka King's College London unaonyesha kuwa kupunguza kiwango cha sukari kwenye damu na kuirejesha katika hali ya kawaida—yaani kuondoa prediabetes—ndiko kunapunguza kwa kiasi kikubwa hatari ya magonjwa ya moyo, si mabadiliko ya mtindo wa maisha pekee kama ilivyodhaniwa awali.

Utafiti huu, uliochapishwa Desemba 2025 katika jarida mashuhuri la The Lancet Diabetes & Endocrinology, umebaini kuwa watu walioweza kurejesha sukari yao ya damu katika viwango vya kawaida walipunguza hatari ya kufa kutokana na ugonjwa wa moyo au kulazwa hospitalini kwa kushindwa kwa moyo kwa zaidi ya asilimia 50.

Matokeo haya yanatajwa kuwa ya kihistoria, kwa kuwa yanapingana na dhana iliyokuwepo kwa miaka mingi katika tiba ya kinga.

Prediabetes ni hali ambapo kiwango cha sukari kwenye damu huwa juu kuliko kawaida lakini bado hakijafikia kiwango cha kuitwa kisukari aina ya pili.

Ingawa watu wengi hujua kuwa prediabetes inaweza kuendelea na kuwa kisukari, wachache hutambua kuwa hali hii pia huongeza hatari ya magonjwa ya moyo, ambayo ni miongoni mwa visababishi vikuu vya vifo duniani.

Takwimu zinaonyesha kuwa nchini Uingereza takribani mtu mmoja kati ya watano ana kisukari au prediabetes. Marekani, ni zaidi ya mtu mmoja kati ya watatu, huku nchini China ikiwa karibu watu wanne kati ya kumi. Kwa ujumla, zaidi ya watu bilioni moja duniani wanakadiriwa kuwa na prediabetes.

Watafiti walifanya uchambuzi upya wa data kutoka tafiti mbili kubwa na za muda mrefu Marekani na China zilifuatilia watu wenye prediabetes kwa miongo kadhaa, huku wakihamasishwa kufanya mazoezi zaidi na kula lishe bora.

Matokeo yalionyesha kuwa watu walioshusha sukari walipunguza hatari ya kufa kutokana na ugonjwa wa moyo au kulazwa kwa kushindwa kwa moyo kwa asilimia 58. Cha kushangaza zaidi ni kwamba manufaa haya yaliendelea kuonekana hata miaka mingi baada ya sukari kurejea katika kiwango cha kawaida, jambo linaloashiria kuwa udhibiti wa mapema wa sukari una athari ya kudumu kwa afya ya moyo.

Zaidi ya hayo, utafiti ulibaini kuwa hatari ya kupata mshtuko wa moyo, kiharusi na matatizo makubwa mengine ya mishipa ya damu ilipungua kwa asilimia 42 kwa wale waliofanikiwa kushusha sukari. Matokeo haya yalikuwa sawa kwa washiriki wa Marekani na China, jambo linaloonyesha kuwa hitimisho hili linaweza kutumika katika jamii na tamaduni tofauti.

Kinyume chake, uchambuzi wa awali wa tafiti hizi ulionyesha kuwa mabadiliko ya mtindo wa maisha pekee—kama mazoezi na lishe bora—hayakupunguza kwa kiasi kikubwa magonjwa ya moyo bali muhimu ni . mabadiliko ya kimetaboliki, hususan kurejesha sukari katika kiwango cha kawaida.

Akizungumzia matokeo hayo, Dkt. Birkenfeld alisema utafiti huu "unapinga moja ya dhana kubwa zaidi katika tiba ya kinga ya kisasa." Alisisitiza kuwa ingawa mazoezi na lishe bora ni muhimu kwa afya kwa ujumla, ushahidi unaonyesha kuwa kushusha sukari ndio kipimo muhimu kinacholinda moyo dhidi ya madhara makubwa na vifo vya mapema.

Kwa mujibu wa watafiti, ugunduzi huu unafanya kushusha sukari ndio nyenzo mpya muhimu ya kinga ya msingi, sambamba na hatua nyingine zinazojulikana kama kupunguza shinikizo la damu, kupunguza kiwango cha mafuta mabaya kwenye damu, na kuacha uvutaji wa sigara. Hivyo basi, utafiti huu unaweza kubadilisha namna madaktari wanavyowashauri na kuwahudumia watu wenye prediabetes.

Kwa ujumla, ujumbe wa utafiti huu ni wazi: lengo kuu kwa mwenye sukari au dalili za kupata sukari halipaswi kuwa tu kupunguza uzito au kufanya mazoezi, bali ni kudhibiti sukari ya damu hadi irejee katika kiwango cha kawaida. Hatua hii inaweza kuokoa maisha, kupunguza mzigo wa magonjwa ya moyo, na kuboresha afya ya jamii kwa kiwango kikubwa.

Sikiliza Radio
Imaan FM
Dar es Salaam 104.5fm
Arusha 90.8fm
Mwanza 106.5fm
Mbeya 90.3fm
Tabora 101.6fm
Ruvuma 94.2fm
Mtwara 90.9fm
Kigoma 92.5fm
/radioimaanfm
MOROGORO
96.3 fm
MSAMVU
twiga
Elimu Bila Mipaka

MATUKIO YENYE MAZINGATIO

NA ZAHARANI BARAKA

Salaf walivyokemea rushwa na ubadhirifu wa mali za umma

Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) alimpeleka Abdullahi bin Rawaha kwa watu wa Khaybar ili akadirie mapato ya mazao yao ya matunda na mazao mengine yanayopatikana katika mashamba yao, lakini wakazi wa Khaybar (Mayahudi) wakajaribu kumpa rushwa ili asifanye uadilifu katika makadirio hayo.

Abdullahi akawaambia: "Wallahi, nimetoka kwa yule ninayempenda zaidi kuliko viumbe wote, na nyinyi mnanichukiza zaidi kwa wingi wenu kuliko nyani na nguruwe. Lakini mapenzi yangu kwake, wala chuki yangu kwenu havitanifanya niache kuwa muadilifu kwenu." ***[Imenukuliwa na Abu Daudi na Ibn Majah].***

Mafundisho ya tukio

Watumishi wengi wanaopewa dhamana ya kusimamia mali za umma hutazama zaidi maslahi yao binafsi, kupokea rushwa, hongo na udanganyifu kuliko kuchunga uadilifu, ukweli na uaminifu wa dhamana waliyopewa.

Abdullahi bin Rawaha (Allah amridhie) ni mfano bora wa kiongozi anayefaa kuaminiwa na kupewa dhamana ya utumishi wa watu. Kwa sababu ya uadilifu na ukweli wake unaotanguliza mbele maslahi ya umma kuliko maslahi binafsi, Abdullahi alikataa rushwa na kusimamia haki ili apate mapato sahihi yatakayosaidia huduma za jamii.

Ilikuwa ni sehemu ya makubaliano kati ya Mtume (rehema na amani zimshukie) na watu wa Khaybar kuwa watatoa nusu ya mapato ya mazao yao yanayotokana na mashamba aliyowakodishia. Rushwa haikuwa na nafasi kwa watumishi waliopewa dhamana ya uongozi na Mtume (rehema na amani zimshukie).

Hakuna ujamaa kwenye uongozi

Baadhi ya watumishi hutumia nyadhifa walizopewa kunufaisha familia zao kwa mazingira ya namna yoyote ile, hata kwa njia ya dhuluma. Jambo hili halikupewa nafasi katika nyakati bora za uongozi wa Masahaba.

Siku moja Ju'dah bin Hubayrah (Allah amrehemu) alikuja kwa Ali bin Abi Twalib (Allah amridhie) akasema: "Ewe Amir wa Waumini, mara nyingi wanakujia watu wawili kwako (kushtakiana), mmoja anakupenda zaidi kuliko anavyoipenda familia yake na mali yake, na mwingine lau angeweza kukuchinja angelikuchinja. Je, utamhukumu huyu dhidi ya yule?" Ali akasema: "Hili ni jambo ambalo lau lingekuwa mikononi mwangu ningefanya hivyo, lakini kwa hakika hili ni jambo la Mwenyezi Mungu." [Imetajwa na Ibn Kathir katika Al–Bidayah Wan–Nihayah].

Kiongozi ni sehemu ya anaowaongoza

Si sahihi kwa kiongozi kujiweka kwenye daraja ya kipekee na kuwaona wale anaowaongoza kuwa ni watu wa tabaka la chini. Kiongozi anatakiwa kuhisi maumivu, taabu, raha na yale yote wanayopitia wale anaowaongoza.

Katika khutba yake ya kwanza baada ya kushika wadhifa wa Ukhalifa, Umar bin Abdul–Aziz (Allah amridhie) alianza kumshukuru Mwenyezi Mungu na kumsifu, kisha akasema: "Baada ya hapo, hakika hakuna Nabii baada ya Nabii wenu, na hakuna kitabu baada ya Kitabu kilichoteremshwa kwake. Fahamuni kwamba alichohalalisha Mwenyezi Mungu ni halali mpaka Siku ya Kiyama, na alichokiharamisha ni haramu mpaka Siku ya Kiyama.

"Fahamuni kuwa mimi si hakimu (mtunga sheria) bali ni mtekelezaji tu. Mimi si mbunifu wa mambo mapya bali ni mfuataji. Fahamuni kuwa hakuna kiumbe anayeruhusiwa kutiiwa katika kumuasi Mwenyezi Mungu. Fahamuni kuwa mimi si bora kuliko nyinyi bali mimi ni mmoja wenu; isipokuwa Mwenyezi Mungu amenifanya nibebe mzigo mzito zaidi kuliko nyinyi." [Ibn Sa'ad katika At–Tabaqat].

Katika khutba hii ambayo ni kama katiba ya utawala wake, na mfano wa kiongozi anayejitolea kuwaongoza watu kwa haki, Umar bin Abdul–Aziz alieleza misingi ambayo utawala wake ungejengwa juu yake. Misingi hiyo ni kuongoza kwa kufuata na kutekeleza sharia ya Mwenyezi Mungu bila ubaguzi, kufuata Sunna sahihi na kuacha uzushi (bid'a).

Hivyo, hakuna kumtii kiumbe katika kumuasi Mwenyezi Mungu, kwa sababu utiifu unaruhusiwa katika mambo yaliyo mema tu. Kiongozi hatofautiani na raia wake kwa chochote, na wala si bora kuliko wengine, bali yeye ni sehemu ya anaowaongoza.

Na huenda miongoni mwa anaowaongoza yupo aliye bora kuliko yeye, na yote haya ni katika njia ya kufikia haki na kuwahurumia raia. Kwa kufanyia kazi misingi hii, Umar (Allah amrehemu) alikuwa akiwaambia watu: "Rudini katika miji yenu, kwa sababu mimi nawataja ninyi mkiwa katika miji yenu na nawasahau mkiwa karibu nami. Fahamuni kuwa nimewaweka watu (viongozi/watumishi) juu yenu, sisemi kuwa wao ni bora kwenu, bali ni bora kuliko wale walio wabaya zaidi kuliko wao.

"Na yeyote atakayedhulumiwa na mtendaji wake, basi hana ruhusa kwangu (ya kunyamaza). Wallahi, lau ningejinyima mimi na watu wa familia yangu mali hii kisha niwanyime na nyinyi, basi ningekuwa mchoyo. Wallahi, lau si kwa ajili ya kufufua Sunna au kutekeleza haki, nisingependa kuishi hata muda mfupi." [Taz: 'Ibn Sa'ad', juz. 5, uk. 253].

Haki na busara huwabadilisha watu

Umar bin Abdul–Aziz alikuwa anaona kuwa, kurekebisha hali iliyoharibika katika nchi/jamii kunapatikana kwa haki na kwa mwongozo wa sharia, si kwa kukandamiza watu, kuwadhalilisha au kutumia sheria za dharura.

Imam Suyuti ametaja katika Taarikh al–Khulafa kutoka kwa Yahya al–Ghassani, ambaye amesema: "Umar bin Abdul–Aziz aliponifanya kuwa Gavana wa Mosul, nilifika huko na kukuta ni miongoni mwa miji yenye wizi na uvamizi mwingi, nikamwandikia barua nikimjulisha hali ya mji na nikamuuliza, 'Je, niwachukulie watu kwa tuhuma, niwapige kwa mashaka, au nichukue kwa ushahidi kama ilivyo katika Sunna?"

IDARA YA DAAWA

Mtume ﷺ amesema:

"Muislamu ni yule ambaye Waislamu wengine wamesalimika kutokana na ulimi wake na mkono wake, na Muhajir (mhamaji wa kweli) ni yule anayeacha kile alichokataza Mwenyezi Mungu."

Bukhari

www.islamicftz.org

JUNAYNAT ALLY DAMA

Hatari ya kujilinganisha na wengine kidini na kidunia

Katika dunia ya leo, tabia ya kujilinganisha na wengine imekuwa chanzo kikubwa cha huzuni, msongo wa mawazo na kupungua kwa thamani binafsi.

Teknolojia, mitandao ya kijamii, na matarajio ya kijamii yamefanya kila mtu atazame maisha ya mwenzake—mafanikio yake, mali alizonazo, hata sura ya maisha yake ya kifamilia—na kujiuliza: "Kwa nini maisha ya kila mtu yanaonekana bora kuliko yangu?"

Kwa mtazamo wa Kiislamu na kimtazamo wa maisha ya kawaida, kujilinganisha kunabeba hatari kubwa kiakili, kihisia na kiroho.

Je, nini hutokea tunapojilinganisha?

Mtaalamu Albert Ellis anasema chanzo cha wivu na maumivu mengi ya ndani ni namna potofu ya kufikiri ambapo mtu haoni uzuri wa maisha yake na kuona mazuri tu ya wengine na hivyo kujihisi mdogo, asiyefanikiwa na asiye na thamani.

Kwa mtazamo wa Kiislamu, wivu na hasad ni miongoni mwa maovu yaliyokuwepo tangu mwanzo wa historia ya mwanadamu. Qur'an inasimulia kisa cha Qabil na Habil—wivu ukampelekea Qabil kutenda kosa kubwa la kumuua ndugu yake.

Hii ni ishara kuwa kujilinganisha kunaweza kuharibu moyo, mahusiano, na hata kumpeleka mtu katika maovu makubwa. Ndani ya moyo huzuka uzito, sononа na wasiwasi, hasa pale mtu anapoona wengine wakipata kile ambacho yeye hana.

Chanzo cha kujilinganisha

Kujilinganisha sio tu tatizo la kijamii; mara nyingi lina mizizi katika mambo yafuatayo:

Chanzo cha kwanza ni mtu kujiona duni, hafai, hana uwezo, au hana sifa fulani zinazothaminiwa na jamii. Hii huchochewa na malezi magumu, unyanyasaji, kupuuzwa kihisia au kushindwa katika malengo muhimu maishani. Hivyo anapoona mwingine akiwa na mafanikio fulani, picha ya nafsi yake huzidi kuwa hafifu.

Pili, kutokuelewa baraka za Allah. Shetani humdanganya mtu aone kuwa alichonacho si kitu. Anapohisi wivu mkali, mtu huhoji kwa nini Allah amempa mwingine uzuri, mali, au afya, na si yeye. Hali hii inavuruga kuridhika na Qadr ya Allah na kupelekea kukosa shukrani.

Sababu ya tatu ni matarajio yasiyo halisi kuhusu maisha. Mara nyingi tunadhani kuwa kuwa na utajiri zaidi, sura nzuri zaidi, au hadhi kubwa zaidi ndiyo njia pekee ya kupata furaha.

Hata hivyo, uhalisia wa maisha ni kwamba kila mwanadamu ana mtihani wake, na hakuna anayeishi maisha kamili kama yanavyoonekana nje.

Mitandao ya kijamii: Jukwaa la taswira bandia

Katika zama hizi, watu huweka mafanikio yao mtandaoni—safari, nyumba nzuri, sherehe, tuzo, ndoa, uzazi n.k. Lakini ni mara chache sana huweka huzuni, migogoro ya kifamilia, deni walilonalo, au changamoto wanazopitia.

Hivyo tunapoangalia maisha ya wengine mtandaoni, mara nyingi tunaangalia sehemu ya juu ya barafu, si uhalisia mzima.

Jinsi ya kujiepusha na tabia ya kujilinganisha

Mosi, tambua thamani yako ya kipekee. Kama alivyonukuliwa Viktor Frankl, kila mtu ana majukumu na nafasi yake ya kipekee duniani ambayo haiwezi kutekelezwa na mwingine.

Pili, jenga mtazamo sahihi wa maisha. Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alitufundisha: "Angalieni wale walio chini yenu, wala msitazame walioko juu yenu ili msizibe baraka za Allah." Hii haimaanishi usijitahidi, bali ujifunze kutambua neema ulizonazo.

Tatu, shukuru neema za Allah kwani utafiti wa kisayansi unaonyesha kuwa kutaja neema ulizonazo kila siku hupunguza wasiwasi na huongeza furaha. Qur'an pia inathibitisha: "Mkiwa na shukrani, hakika Nitakuzidishieni." [Quran,14:7].

Nne, jiwekee mipaka ya kulinganisha. Ikiwa lazima ujilinganishe, basi jilinganishe na wewe wa jana, na kamwe usijilinganishe na watu wengine. Jiulize, je, umeimarika kiroho? Kitaaluma? Kifamilia? Kiuchumi? Huu ndio mlinganisho mzuri.

Tano, jiboreshe. Badala ya kutumia saa mbili kwa siku kutazama maisha ya wengine, tumia muda huohuo kuboresha ujuzi wako, kusoma Qur'an, kufanya mazoezi au kutafuta riziki halali. Maisha yanabadilika unapofanya hatua ndogo ndogo kila siku.

Nimalize kwa kusema kuonya kuwa kujilinganisha kupita kiasi ni sumu ya akili, moyo na roho. Kunapunguza thamani binafsi, kunazidisha huzuni, na kunaweza kumkosesha mtu mtazamo sahihi wa neema za Allah. Uislamu unatufundisha kuishi kwa shukrani, kutoridhishwa na dhana ya dunia tu, na kuamini kuwa riziki na baraka zimegawiwa kwa hekima ya Mola.

UKHTI FATIMA SS

Una akili ya maisha au akili ya darasani?

Katika maisha ya kila siku tunakutana na kauli kama, "Fulani ana akili sana darasani," au "Yule ana akili za maisha." Kauli hizi zinatufundisha jambo moja muhimu: akili si kitu kimoja tu. Ina sura nyingi tofauti, na kila mtu ana kipawa chake cha kipekee.

Wapo ambao hawakufanya vizuri shuleni lakini wamefanikiwa maishani kuliko hata wale waliokuwa vinara madarasa. Hii inaonyesha kuwa akili ya mtu haiwezi kupimwa kwa mtihani pekee, bali kwa namna anavyotumia uwezo wake kutatua changamoto za maisha.

Akili: nini maana yake?

Akili ni uwezo wa kujifunza, kufikiri kwa mantiki, kutatua matatizo, kujenga uhusiano kati ya maarifa na mazingira, na kutumia uzoefu kufanya maamuzi bora.

Hata hivyo, jinsi ya kufasiri aina za akili imekuwa mjadala wa muda mrefu. Charles Spearman aliona akili kama kitu kimoja kikuu kinachoitwa g–factor. Wataalamu wengine kama Howard Gardner waliamini kuwa akili ina aina nyingi, ambapo mtu anaweza kuwa dhaifu kwenye eneo moja lakini akang'ara sana eneo lingine.

Katika maisha, tunashuhudia mtoto mdogo anayejifunza kusoma haraka kuliko umri wake, au mtu mzima anayeweza kubuni suluhisho la tatizo bila msaada wa vitabu. Haya yote ni mifano ya namna tofauti za akili zinavyojitokeza.

Nadharia ya Sternberg: aina tatu kuu za akili

Mtaalamu Robert Sternberg alitoa maelezo muhimu kuhusu akili kupitia nadharia yake ya 'triarchic', akisema kuwa akili ina sehemu tatu kuu zinazotumiwa kila siku bila kujitambua.

Mosi, kuna akili ya uchanganuzi. Hii ndiyo akili inayofanana na uelewa wa masomo ya darasani. Mtu mwenye aina hii ya akili ana uwezo wa kuchambua hoja, kufanya mlinganisho, kuelewa mifumo, na kutatua maswali magumu ya nadharia. Wanaofanya vizuri kwenye mitihani au kwenye utafiti mara nyingi hutumia akili hii.

Pili, kuna akili ya ubunifu. Huu ni uwezo wa kubuni mawazo mapya, kufikiria nje ya mipaka na kupata majibu yasiyo ya kawaida. Ubunifu hauhusiani tu na sanaa; unaweza kuonekana kwenye teknolojia, biashara, uandishi, au hata kutatua tukio lisilotarajiwa. Mfano ni mtu anayejua kufikiria njia mbadala za kukabiliana na changamoto bila kukata tamaa.

Tatu, kuna akili ya utendaji. Hii mara nyingi huitwa "akili za maisha." Ni uwezo wa kutumia maarifa katika mazingira ya kawaida. Mtu huyu anaweza kusoma hali ya watu, kupanga ratiba vyema, kupata fursa kirahisi au kujua cha kufanya panapotokea tatizo. Watu wenye akili hii wana ufanisi mkubwa kwenye kazi za vitendo, uongozi, biashara na mawasiliano ya kijamii.

Kwa kuangalia mifano mbalimbali, inakuwa wazi kwamba akili ya uchanganuzi inaweza kukusaidia kufaulu mitihani, lakini akili ya ubunifu na utendaji mara nyingi ndiyo msingi wa mafanikio ya maisha halisi.

Akili ya hisia (emotional intelligence)

Aina nyingine muhimu ni akili ya hisia. Huu ni uwezo wa kuelewa hisia zako na za wengine, kujidhibiti unapokasirika, kuonyesha huruma, na kujua namna ya kukabiliana na migogoro. Watu wenye aina hii ya akili wanapendwa, wanaongoza vyema na wana uwezo wa kufanya kazi na watu wenye tabia tofauti.

Watafiti kama Daniel Goleman wamedai kuwa akili ya hisia mara nyingi inatabiri mafanikio kuliko hata IQ ya kawaida. Hii ni kwa sababu mahusiano ndiyo msingi wa maisha yetu—katika kazi, ndoa, biashara na hata urafiki. Mtu anayeweza kuelewa hisia ana uwezo mkubwa wa kushirikiana na wengine, kujenga mitandao ya kijamii na kufikia malengo yake.

Aina nyingine za akili

Raymond Cattell alieleza kuwepo kwa aina mbili za akili zinazosaidiana. Akili ya mfululizo ni uwezo wa kutatua matatizo mapya kwa harakaikitumika kutatua tatizo lisilotarajiwa. Pili ni akili ya yaliyohifadhiwa, yaani maarifa uliyojifunza kutokana na uzoefu, elimu au mazoea.

Howard Gardner aliongeza wigo akitaja angalau aina nane za akili: ya lugha, mantiki na hesabu, mwili na harakati, kuona na kutengeneza picha, muziki, kijamii, kujitambua na akili ya asili. Lengo la Gardner lilikuwa kuonyesha kuwa kila mtu ana kipawa chake cha kipekee ambacho kinaweza kuendelezwa na kuleta mafanikio.

Kwa ujumla, akili si kipimo cha mtihani bali ni uwezo wa mtu kutumia vipawa vyake kutatua changamoto za maisha, kubuni mambo mapya na kujenga mahusiano bora. Kila mtu ni mwenye akili, ila akili hiyo inahitaji kutambuliwa, kuendelezwa na kutumiwa ipasavyo.

Tathmini afya ya uchumi wako binafsi

Afya ya kifedha ni msingi wa ustawi wa maisha ya mtu katika zama hizi. Kama ambavyo tunachukua muda kupima afya ya miili yetu, ndivyo tunavyopaswa pia kupima hali ya uchumi wetu binafsi ili kuhakikisha tuko katika njia salama.

Mtu anaweza kuonekana anaishi vizuri nje, lakini ndani anapambana na madeni, matumizi yasiyodhibitiwa, au kukosa akiba ya dharura. Uislamu unatufundisha kuishi kwa nidhamu, kutopindukia katika matumizi, na kujiepusha na madeni yasiyo ya lazima.

Hivyo, kujua afya yako ya kifedha si anasa; ni jukumu la kiimani na msingi wa maisha yenye utulivu. Katika makala hii, tutachunguza hali yako ya kutathmini hali yako ya kiuchumi.

Je, ukoje kwenye vigezo hivi?

Kuna mambo kadhaa muhimu yanayoonyesha afya yako ya kifedha kwa ujumla. Ingawa hakuna kipimo kimoja kinachotosha, mkusanyiko wa viashiria hivi unatoa taswira halisi ya ustawi wako wa kiuchumi.

Mosi, kokotoa thamani yako

Hii ndiyo picha ya kweli ya hali yako kifedha. Unachofanya ni kukokotoa tofauti kati ya kile unachomiliki na kile unachodaiwa. Ikiwa mali zako za halali kama akiba, nyumba, au vitega uchumi vinazidi madeni yako, upo katika hali nzuri.

Ikiwa madeni yanazidi mali, basi ni ishara ya kuanza kuchukua hatua za kupona kiuchumi. Kwa mtazamo wa Kiislamu, msingi ni kutumia mali kwa halali, kuepuka riba, na kudhibiti matumizi ili usiingie katika dhiki zisizo za lazima.

Pili, unatunza asilimia ngapi ya kipato chako?

Kiwango hiki kinaonyesha asilimia ya kipato unachoweka akiba kwa ajili ya baadaye. Kutunza fedha ni msingi wa amani ya kifedha. Mtu anayejitahidi kuweka akiba anakuwa na uwezo wa kukabiliana na dharura bila kuingia katika mikopo isiyofaa.

Kama huwezi kuweka akiba hata kidogo kila mwezi, ni dalili kuwa matumizi yanahitaji kufanyiwa marekebisho.

Tatu, linganisha madeni na kipato.

Hii ni njia ya kuangalia kama mzigo wa madeni unafaa au unakulemea. Ikiwa sehemu kubwa ya kipato chako inaishia kulipa madeni ya nyuma, basi afya yako ya kifedha imeathirika.

Uislamu unahimiza kulipa madeni mapema na kuepuka kujilimbikizia wajibu unaoweza kukuweka katika presha au kukuzuia kutimiza ibada na majukumu mengine ya maisha.

Nne, umejiandaaje kwa ajili ya uzeeni?

Kustaafu si tukio la ghafla. Ni safari inayohitaji maandalizi ya mapema. Mtu anapaswa kuwa na mpango wa muda mrefu unaoendana na kipato chake, bila kutegemea mikopo au mifumo yenye mashaka ya kifedha. Ikiwa huna mpango wa baadae, basi ni ishara kuwa unahitaji marekebisho haraka.

Tano, una akiba ya kukabiliana na dharura?

Kuwa na akiba ya dharura inayotosha angalau miezi kadhaa ya matumizi ni ishara kuwa una ustawi wa kifedha. Hii inakupa uwezo wa kukabiliana na changamoto kama ugonjwa, kupoteza kazi, au dharura nyingine bila kuingia kwenye madeni yasiyo halali. Uislamu unahimiza kujitayarisha kabla ya shida na kutumia neema kwa hekima.

Je ufanyeje?

Baada ya kujua hali yako ya kifedha, hatua inayofuata ni kuboresha afya hiyo kwa njia zinazoendana na misingi ya Kiislamu.

Mosi, tengeneza na fuata bajeti ya matumizi. Bajeti hukupa uwezo wa kudhibiti mali uliyopewa na Mwenyezi Mungu. Inakusaidia kutenganisha mahitaji ya lazima na matumizi ya ziada.

Pili, dhibiti madeni na epuka mikopo yenye riba. Ikiwa unalo deni, lipa kwa wakati na kwa uwazi. Ukikopa, hakikisha ni kwa dharura halisi na katika njia halali. Kuepuka riba ni msingi wa uadilifu wa kifedha katika Uislamu.

Tatu, jenga mfuko wa dharura. Kuweka akiba ya miezi 3–6 kunapunguza wasiwasi na kukuweka huru dhidi ya kushindwa kukidhi mahitaji muhimu wakati wa dharura. Ni kinga muhimu ya kiuchumi na kimaadili.

Nne, wekeza katika njia za halali kwa ajili ya mustakabali. Jifunze kuhusu uwekezaji unaoendana na masharti ya Kiislamu, kama kushiriki katika biashara halali au miradi inayokidhi kanuni za kifiqhi. Uwekezaji hutoa fursa ya kukua kiuchumi bila kuvunja mipaka ya dini.

Tano, panga maisha yako ya baadaye. Tathmini mahitaji ya familia, elimu ya watoto, makazi, na maandalizi ya uzee. Uislamu unahimiza kupanga kabla ya wakati, bila kutegemea bahati au miujiza.